SportPesa
TZS. 595,659,980
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Chanjo** Johnson & Johnson kuisha ndani ya wiki moja

UKURASA 3



**Aguero atoa neno kuanza kukipiga Barcelona**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumanne Oktoba 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0580738

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Mwonekano, maisha mapya ya Ole Sabaya

• **Mashahidi** waomba atoe barakoa kumtambua... *Uk. 2 na 19*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### SAMIA AJIVUNIA SAFARI ZA NJE

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema kuwa ataendelea kutumbua na kwamba wananchi wakisikia...

**UKURASA WA 4**

### TANROADS YABANWA MATUMIZI BIL. 600/-

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imeuagiza Wakala wa...

**UKURASA WA 5**

### WAZIRI WA UFARANSA KUTUA NCHINI KIUTALII

WAZIRI wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Kiuchumi wa Ufaransa...



Eneo la Chuo cha Biashara jijini Dar es Salaam ambalo lilikuwa limezingirwa na wafanyabiashara wadogo (machinga) likiwa wazi jana, baada ya kuondoka kwa hiari yao kutokana na amri ya serikali ya mkoa kuwataka waondoke. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bugando yazuia maiti

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (kushoto) na Mkuu wa Idara ya Huduma za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo (wapili kulia), wakati wa uzinduzi wa Kiwanda cha Nyama cha Eliya Food kilichoko Kimokouwa, Namanga wilayani Longido jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Wamachinga waongezewa siku 12 Dar, Samia apongeza

UKURASA 3

Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

**MICHEZO** NABI ATEMA CHECHE KIWANGO YANGA, KMC UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mwonekano, maisha mapya ya Ole Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MWONEKANO na maisha mapya ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, jana uliwachanganya mashahidi wa nne na wa tano kulazimika kuiomba Mahakama atoe barakoa ili wamtambue.

Tofauti na kabla ya hukumu ya Oktoba 15, mwaka huu, mshahidi waliofika mbele ya mahakama hiyo walimtambua kwa urahisi kwa kuwa mwonekano wake ulikuwa ni ule ule wa wakati akiwa kiongozi na kuonekana kwenye vyombo vya habari.

Jana Sabaya alitinga mahakamani humo akiwa amenyolewa upara ilhali mwonekano wake ni kunyoa panki, pia alinyolewa ndevu na kawaida yake ni mwenye ndevu maarufu kama mzuzu.

Mabadiliko hayo yamesababishwa na kuwa Sabaya kwa sasa ni mfungwa aliyehukumiwa jela miaka 30 baada ya Mahakama kumkuta na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Kwa mujibu wa taratibu za Magereza, mtu anapokuwa mfungwa hunyolewa kipara, na ndicho kilichotokea kwa Sabaya ambaye bado anakabiliwa na kesi nyingine ya uhujumu uchumi na kutakiwa kuhudhuria mahakamani kila tarehe ya kesi husika.

Ole Sabaya na wenzake wawili Silvester Nyegu na Daniel Mbura, Oktoba 15, mwaka huu, walihukumiwa kifungo cha miaka 30 kwenda jela.

Katika kesi ya uhujumu uchumi mbali na Sabaya washtakiwa wenzake sita ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29), Nathan Msuya(31) wanakabiliwa na mashtaka matano.

Ilizoeleka kwa mshtakiwa huyo kunyoa panki na kuachia ndevu mithili ya mzuzu, lakini vyote hivyo jana havikuwapo kwa kuwa alikuwa amenyoa ndevu na nywele upara.

Mwonekano mpya wa Sabaya ulimfanya kuwa wa tofauti hadi mashahidi wa nne na  wa tano katika kesi ya uhujumu uchumi walishindwa kumtambua hadi kuiomba mahakama washtakiwa hao kuvua barokoa ili waweze kuwatambua.

Awali, wakati wa kuanza kusikilizwa kwa kesi zote mbili ambazo ni ya jinai namba 105 na uhujumu, mshtakiwa huyo alikuwa akiwapungia waliofika mahakamani humo na kuongea mawili matatu na ndugu jamaa na marafiki.

Kwa siku ya jana hali ilikuwa tofauti kwa kuwa hakuwa na uchangamfu kama aliokuwa nao nyakati za nyuma, bali alipunga mara moja na kuingia mahakamani kwa upole.

Nyakati za nyuma alionekana kuwa na ujasiri jana hakuonyesha uso uliochangamka kama kawaida bali alijawa na huzuni.

Vile vile, mahudhurio ya watu katika kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi yamepungua ukilinganisha na kwenye kesi ya jinai iliyomalizika Oktoba 15, mwaka huu.

Pia, ndugu za washtakiwa hao wameonekana kutokuwa na furaha ukilinganisha awali kabla ya hukumu hiyo.




Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, akiongoza kikao cha Tume ya Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji inayoshughulikia masuala ya kiutumishi na kiutendaji wa askari katika majeshi hayo, katika ukumbi wa wizara hiyo, jijini Dodoma, jana. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Maiti yazuiwa Bugando kisa deni

**Na Richard Makore,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Bugando jijini Mwanza, imedaiwa kuzuia maiti ya Rosemary Morumbe, mkazi wa kijiji cha Kerukerege wilayani Serengeti mkoani Mara, kutokana na kudaiwa Sh. milioni 2.4  za matibabu.

Marehemu Rosemary alifariki dunia usiku wa wiki iliyopita na mwili wake ukahifadhiwa hospitalini hapo kusubiri ndugu kwa ajili ya mazishi.

Mmoja wa ndugu wa marehemu, Scola Marungu, akizungumza na Nipashe, alisema ndugu yao alitibiwa hospitalini hapo kwa kipindi kirefu na kwamba gharama zote zilikuwa Sh. milioni 6.9.

Alisema familia ilitafuta fedha ikalipa Sh. milioni 4.4,  na kwamba zikabaki zaidi ya Sh. milioni ambazo wameshindwa kuzilipa mpaka sasa.

Alisema Jumapili asubuhi alifika hospitalini hapo na kuambiwa na wauguzi kwamba ndugu yao alifariki dunia usiku wa iliyopita na mwili wake umehifadhiwa chumba cha maiti.

Aidha, alisema licha ya kupewa taarifa hiyo, aliambiwa kwamba ndugu yao anadaiwa zaidi ya Sh. milioni 2 ambazo zinatakiwa kulipwa ili wapewe mwili wa marehemu kwa ajili ya mazishi.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Tiba wa hospitali hiyo, Dk. Bahati Wajanga, alipoulizwa alisema hajui suala hilo na kuomba kukutana na wanafamilia hao.

"Nipe namba zao niwasiliane nao ili waje ofisini kwangu mimi nipo hapa sasa hivi," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alisema msimamo wa serikali ni kutozuia maiti hospitali kama aliyefariki anadaiwa.

Alisema huo ndiyo msimamo, lakini alisema suala la utekelezaji ni kitu kingine katika hospitali husika.

# Mabilioni ya UVIKO-19 kusaidia kaya 40,740

**Na Elizabeth Zaya**

KAYA 40,740 za walengwa waliopo kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), zinatarajiwa kunufaika na Sh. bilioni 5.5 ambazo zimetoka katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, Ladslaus Mwamanga, alisema watakaonufaika na fedha hizo ni wa kwenye miji na majiji.

"Katika utafiti mdogo tulibaini asilimia kubwa na walengwa wa kaya hizi maskini waliopata athari za corona ni wa mijini hususani kwenye miji na majiji na ndio maana serikali imeamua kutoa hizo fedha kwa ajili kuwasaidia,"alisema Mwamanga.

Mwamanga alisema walengwa watanufaika na pesa hizo kupitia ruzuku na ajira za muda.

"TASAF inatekeleza mpango wa kunusuru kaya za walengwa katika halmashauri 184 za Tanzania Bara, Unguja na Pemba na idadi ya kaya ni milioni 1.4 zenye watu zaidi ya milioni 10 zinazotoka kwenye mazingira magumu na hivyo kupatiwa ruzuku ya kujikimu, kufanya kazi kwenye miradi ya jamii na kulipwa ujira ambao unaziongezea kipato na kuunganishwa kwenye vikundi vya kujiwekea akiba," alisema Mwamanga.

"Baada ya uzinduzi wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF, nchi ilipatwa na janga la UVIKO-19 na kusababisha shughuli nyingi kusimama ili kuzuia maambukizi kwa njia ya mikusanyiko. Kutokana na hali hiyo, walengwa hawakupata fursa ya kukutana wao kwa wao pamoja na wataalam kwa ajili ya kupata maarifa kuhusu lishe, ufugaji, kilimo na shughuli za ujasiriamali na hivyo baadhi yao kujikuta miradi yao ikiharibika na hivyo kuathirika zaidi."

Mwamanga alisema kupitia miradi ya kijamii ambayo walengwa watajipatia ajira za muda kupitia pesa za msaada huo, watakuwa wanalipwa Sh.135,000 kwa kila kaya ambazo ziliathirika zaidi kutoka na ugonjwa huo ili kufufua na kuimarisha shughuli zao za kukuza uchumi wa kaya.

Serikali ya Tanzania imepata mkopo wa Sh. trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kampeni ya Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.




Kamishna wa Uhifadhi Misitu, Prof. Dos Santos Silayo (kulia), akiwa amekaa kwenye madawati ambayo alimkabidhi Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Maajabu Nkanyemka, aliyemwakilisha mkurugenzi, msaada wa madawati 120 yenye thamani ya Sh. milioni 12.6 kwa ajili ya Shule ya Msingi Kipera, iliyoko mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chanjo Johnson & Johnson kuisha ndani ya wiki moja

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema chanjo ya Johnson & Johnson (JJ) imebaki kidogo na ndani ya wiki moja itakuwa imekwisha.

Pia, wameanza kusambaza chanjo mpya ya Sinopharm katika vituo vya afya.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akihojiwa na waandishi wa habari baada ya kufungua mkutano mkuu wa 26 wa mwaka wa Chama cha Madaktari Bingwa wa magonjwa ya kike na uzazi Tanzania (AGOTA).

"Chanjo ya awamu ya kwanza zilizokuja Johnson Johnson karibu zinaisha zimebaki dozi 25,000 hazina siku saba zitakuwa zimeisha, lakini kwa kugundua kuwa katika maeneo mengi ambayo JJ imeisha tumesambaza Sinopharm," alifafanua Gwajima.

Alisema kwa jana tayari baadhi ya vituo vimeshaanza kuchanja chanjo hiyo ya Sinopharm na kuomba wajitokeze kuchanja.

Alisema ugonjwa wa Uviko-19 bado upo, wananchi wanatakiwa kuendelea na mapambano na ambao hawajachanja waende ili kujikinga na maambukizi.

"Hatujasema COVID -19 imekwisha mapambano yale na mbinu tulizozielekeza kila siku tunatakiwa kuzifuata wale ambao hawajachanja waende kuchanja ni mbinu mojawapo ya kupambana na huu ugonjwa na wale waliochanja pia waendelee kutumia zile mbinu za kujikinga," alisema.

Alisema aliyechanjwa akiambukizwa hatakuwa na ugonjwa mkali ikilinganishwa na yule ambaye hajachanja.

**VIFO VYA UZAZI**

Dk. Gwajima alisema serikali imetuma timu ya wataalamu kufanya utafiti wa kujua idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kwa kiwango gani na taarifa itatolewa Desemba mwakani baada ya kukamilika.

Alisema ufuatiliaji wa mwenendo wa hali ya vifo vitokanavyo na uzazi nchini unaonyesha kuwa kufikia mwaka 2020 taarifa zinaashiria kuwa kiwango cha vifo vitokanavyo na uzazi kipo chini ya vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000.

"Kwa wakati huu tunavyozungumza timu ya watafiti ya NIMRI ikishirikiana na taasisi ya Umoja wa Mataifa inayofuatilia hali ya vifo vitokanavyo na uzazi, UDSM, MUHAS, UDOM na KCMco wapo kwenye ukusanyaji wa takwimu elekezi la vifo vitokanavyo na uzazi katika kujitayarisha kukusanya takwimu hizi kwenye mfumo wa utafiti wa kufuatilia vifo vya kinamama walio katika umri wa kujifungua," alisema Waziri.

Alisema Tanzania imepiga hatua kubwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya na wamejenga vituo 487 na kupatiwa vifaa, ikiwamo vya upasuaji wa dharura kwa kumtoa mtoto tumboni.

Alisema ili kuhakikisha vituo hivyo vinatoa huduma bora, anatoa rai kwa vyama vya kitaalamu ikiwamo AGOTA, SATA, TAMA na TANNA kushirikiana na serikali kuhakikisha watumishi wa vituo hivyo wanapata mafunzo, kuwasimamia na kuwafuatilia kuhakikisha wanatumia miongozo katika kutoa huduma za dharura.

Alisema kufuatia maboresho yaliyofanywa katika sekta ya afya, uboreshaji wa huduma za kibingwa idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi imepungua kwa asilimia kubwa na kwa sasa hawazidi wagonjwa 50.

Naye, Daktari bingwa wa wanawake, Profesa Charles Majinge alisema ugonjwa wa Uviko-19 ulivyoingia awali kulikuwa na changamoto baadhi ya madaktari kuwaogopa wagonjwa na wagonjwa kuwaogopa madaktari na wengine hata kujifungulia nyumbani.

Alisema idadi ya wanawake kwenda kliniki ilipungua na sababu ya madaktari kuwaogopa wagonjwa ni kutokana na kukosekana kwa vifaa vya kujikinga wakati Uviko-19 unaingia nchini.

Rais wa AGOTA, Dk. Matilda Ngarina, alisema chama hicho kilianza mwaka 1974 wakiwa wajumbe 10 na hadi sasa wapo wanachama takribani 300.

Alisema malengo yao ni kuwezesha upatikanji bora wa afya ya mwili na akili kwa wajawazito na watoto wachanga, kuhamasisha ubadilishanaji wa mawazo na uzoefu miongoni mwa wataalamu katika eneo la afya ya uzazi na mtoto mchanga kwa kutumia mbinu za kitaalamu zinazokubalika.

Pia, alisema kusimamia ubora na viwango vya mafunzo katika ngazi zote kwenye eneo la afya ya kinamama na uzazi na kuhamasisha utafiti wa kisayansi katika eneo la afya ya kinamama na uzazi.

# Wamachinga waongezewa siku 12 Dar, Samia apongeza

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ameongeza siku 12 kwa wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama machinga kujiandaa kuhamia maeneo waliyotengewa ili kuepuka usumbufu na kurahisisha usafi wa mji.

Amesema baada ya muda huo hatasikiliza kisingizio chochote kutoka kwa wafanyabiashara hao, zaidi ya kuhamia wanakotakiwa na kuondoka kusikotakiwa.

Akizungumza jana na wafanyabiashara katika Soko Kuu la Kariakoo, alisema uamuzi huo umekuja baada ya mwezi mmoja uliotolewa kujiandaa na kuondoka katika maeneo yasiyo rasmi kuisha.

"Nawapa muda mpaka Oktoba 30, baada ya hapo sitaki kusikia kisingizio chochote labda mtu aje na malalamiko kwamba kaenda kwenye maeneo yaliyotengwa kakosa nafasi, wanaotakiwa kuondoka ni wale walio juu ya mifereji na mitaro, hifadhi za barabara na mbele ya shule au taasisi za serikali," alifafanua.

Pia alisema watajadiliana na uongozi wa wafanyabiashara hao na kusisitiza kuwa serikali inawathamini ndiyo maana wametengewa maeneo, kwa mpango wa muda mrefu ni kuliweka jiji hilo kuwa mfano wa kuigwa kwenye usafi barani Afrika.

Aidha, aliagiza eneo la DDC, Kariakoo liboreshwe ili kupokea wafanyabiashara wengi zaidi tofauti na sasa linapotumika kuuza vyakula na vinywaji.

Mkuu huyo wa mkoa alisema ameridhishwa na baadhi ya wafanyabishara hao kuhama kwa hiari maeneo wasiyotakiwa.

Makalla alisema hadi sasa maeneo ambayo wafanyabiashara wameondoka na kufanikiwa kuwa wazi ni Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Maktaba Posta, Vingunguti, Gongolamboto, Mikocheni na Mwenge, na kwamba japokuwa baadhi ya maeneo mama lishe wanaonekana kuvunja vibanda, lakini wakiendelea na biashara kwa kuweka mwamvuli.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Machinga, Steven Lusinde aliomba serikali kuwapeleka kwenye maeneo yaliyo na mwingiliano mkubwa wa watu kuliko na biashara.

"Tunaiomba mamlaka kutekeleza amri kwa makubaliano kwani wafanyabiashara wengi wanayo mikopo na wanategemewa na watoto ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji yao," alisema. Pia, inasadikika kuwa zaidi ya wafanyabiashara 5,000 wataathirika na uamuzi wa mamlaka za miji kwa kuwaondoa maeneo yasiyo rasmi.

Katika Soko la Kariakoo ambako wafanyabiashara zaidi ya 1,500 wanaendesha shughuli zao na kujiingizia kipato kinachowasaidia kumudu gharama za maisha, walisema wanahitaji kuwa na uhakika wa biashara yao katika soko hilo linalohudumia zaidi ya watu 3,000 kwa siku.

Hivi karibuni, akihutubia wakazi wa Jiji la Arusha, Rais Samia Suluhu Hassan, aliipongeza Dar es Salaam kwa kuwapanga machinga kiasi cha kuwezesha maeneo mengi kuonekana vizuri na kurahisisha usafi na kuwataka miji na majiji mengine kuiga.

**KUMBUKUMBU YA KUFIKISHA MIAKA 40 YA KUZALIWA YA MPENDWA WETU MAREHEMU UMMI ABDUL TULI.**



616519902

**Kuzaliwa: Tarehe 19 Oktoba 1981**
**Kufariki: Tarehe 01 Machi, 2003**

Tunamshukuru ALLAH kwa muda aliotujalia kuishi nawe UMMI. Kwa upendo unakumbukwa na Familia za TULI, LUHANGA, NDUGU NA MARAFIKI.

**"AMETUKUKA AMBAYE UKO MIKONONI MWAKE UFALME NA AMBAYE AMEUMBA MAUTI NA UHAI" Quran 67: 1 na 2.**




Mkufunzi wa kutumia mashine ya kuusaidia moyo kufanya kazi kwa kiwango cha juu (Intra-aortic balloon pump) kutoka nchini Afrika Kusini, Linda Veale, akiwaonyesha wataalamu wa afya wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) namna ambavyo mashine hiyo inavyofanya kazi, wakati wa mafunzo yaliyofanyika jana, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JKCI**

# Rais Samia Suluhu ataja mafanikio ziara za nje

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema kuwa ziara zake nje ya nchi ni kwa ajili ya Watanzania na sio kwa lengo la kutembea kwenye nchi hizo.

Akihutubia wananchi jijini Arusha juzi, alisema ziara chache alizofanya nchi mbalimbali zimesaidia kuondoa vikwazo na kuogeza wigo kwa wafanyabiashara nchini.

"Ziara nilizokuwa nikifanya nchi jirani madhumuni ilikuwa kuondoa vikwazo, kunyoosha njia ili wafanyabiashara wetu waweze kuuza ndani na nje, tumeondosha vikwazo na nchi ya Kenya, naambiwa biashara imekuwa mara sita kuliko wakati wa vikwazo," alisema na kuongeza;

"Tukizunguka (ziara za nje) hivi msiseme mama (Rais) anazunguka tu, sitazunguka bila sababu, nilishacheza vya kutosha kwenye nchi nyingi duniani, sasa hivi kazi ni moja tu kuzunguka kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania."

**KUPANDA SARUJI, MABATI**

Rais Samia alithibitisha kupanda kwa bei ya saruji na mabati na tatizo baadhi ya wazalishaji waagiza malighafi nje ambako kulikuwa kumefungwa kutokana na Uviko-19.

"Nimemwagiza Waziri wa Viwanda na Uwekezaji awaite wazalishaji wa saruji, nondo, mabati na vifaa vingine vya ujenzi kwa sababu fedha (Uviko-19) tulizipitisha juzi za ujenzi wa madarasa zaidi ya 15,000 kama vifaa hivyo vitakuwa bei juu mradi wetu utafeli, tunawataka wazalishe bidhaa kwa wingi ili wananchi wapate na bei ishuke," alisema.

**AKUSANYA MABANGO**

Akiwa Usa River kuelekea jijini Arusha, Rais Samia aliagiza mabango yote waliyokuwa wamebeba wananchi yakusanywe na akaahidi kwenda kuyasoma yote.

**MAJI, BARABARA**

Alisema changamoto kubwa ya Mkoa wa Arusha ni barabara na maji na kwamba kitakachofanyika ni kukaa mkoa na wilaya zake ili kuangalia barabara za kipaumbele kuanza nazo kwa zilizoko chini ya TANROADS na TARURA.

"Tunataka zipitike muda wote mazao yatoke shambani kwenda kwenye masoko, tutajipanga vizuri kuangalia wapi kuanze na wapi tumalizie, tunaunganisha wilaya kwa wilaya, kuondoa barabara za vumbi. Miradi ya maji tumeishughulikia inaendelea kukamilika," alisema.

Akiwa jijini Arusha, alisema serikali itafufua viwanda ili kutoa ajira kwa wingi na kukuza uchumi, huku akisema wanarudisha hadhi ya Tanzanite ijulikane inatoka Tanzania na sio kuacha itoke holela bila nchi kuona faida.

Rais Samia alisema kwa muda mrefu watu wengi duniani wanajua madini hayo yanapatikana nchi nyingine badala ya Tanzania na kuhahidi kwamba kwa sasa wanairudishia hadhi na kuna udhibiti ili nchi ione manufaa.

"Tukiachia itoke inavyotoka itakwisha bila kuona thamani yake, kwa sasa tunadhibiti tunaitoa kwa viwango, tunaangalia mahitaji ya ulimwengu na bei ya Tanzanite itapanda kwa sababu tunatengeneza chache katika kupeleka duniani na thamani yake itapanda na nchi itanufaika, na sasa tuna hesabu imechangia kiasi gani kwenye uchumi wetu," alisema.

**MIKOPO YA NJE**

"Nawaahidhi Watanzania nitaangalia mikopo yenye unafuu kwa nchi yetu, inayoleta faida kwa nchi yetu, mikopo chechefu sitaichukua ila inayoleta nafuu na maendeleo sitaiogopa nitaichukua," alisema.

**VIWANDA**

Alisema serikali imejipanga kuanzisha kongamano la viwanda na kwa sasa wanamalizana na mwekezaji wa kiwanda cha matairi ya General Tyre, kwa kuwekeza viwanda zaidi ya 20 ikiwamo cha kutengeneza mpira.

"Viwanda ni ajira kwa Watanzania, serikali iko kwenye mpango wa kuviandalia viwanda vilivyofungwa ni ukweli hata vikifufuliwa leo haviwezi kufanya kazi iliyofanyika wakati huo ndiyo maana tumekuja na kongano za viwanda kila eneo lililofaa ili kukuza ajira na uchumi wa taifa," alisema.

Alihidi kushughulikia migogoro ya ardhi, ujenzi wa barabara kwa ajili ya kuharakisha maendeleo na mkopo wa kushughulikia utalii, afya na elimu.

"Tunataka kuhakikisha matatizo yote yanayowakabili wananchi tunayashughulikia ipasavyo, tuna tatizo la wafanyabiashara wadogo na masoko, yote tunayafanyia kazi ili wananchi waondokane na kero... lengo letu ni kuwahudumia wananchi, tunachoomba amani na utulivu serikali yenu ipo na kwa ajili ya wananchi," alisema.

# Kibano TANROADS kutumia bil. 600/- bila kibali cha Bunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imeuagiza Wakala wa Barabara (TANROADS) kuwasilisha maelezo ya kina ya kimaandishi kuhusu matumizi ya Sh. bilioni 616.3 bila idhini ya Bunge.

Sambamba na hilo, imewatimua watendaji wa wakala huo katika kikao kutokana na kutowasilishwa kwa wakati nyaraka zilizopaswa kufanyiwa kazi na kamati hiyo kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka alisema wakala huo katika hoja za ukaguzi zinazoishia Juni 30, mwaka 2020 umefanya matumizi mabaya ya Sh. bilioni 616.3 kinyume cha taratibu bila kuidhinishwa na Bunge na kutaka majibu ya hoja zilizoibuliwa kuwasilishwa kesho.

Alisema haiwezekani kutumia fedha ya umma zaidi ya ile iliyopitishwa kwenye bajeti kama hawajapata kibali cha Bunge.

"Tumewaagiza watuletee kwa maandishi aliyeidhinisha kutumika kwa kiasi hicho cha fedha na kufanya matumizi hayo bila kibali cha bunge," alisema.

Kuhusu kutofanyika kikao, Kaboyoka alisema "nyaraka huwasilishwa na CAG lakini tumezipata tukiwa kwenye kikao, tulijua kwamba hatutaweza kutendea haki kazi hii kutokana na kwamba Sheria ya Bunge ambayo inatufanya tufanye vikao inataka kwamba nyaraka zote, ripoti ya CAG kuhusu miradi mbalimbali ambayo tunasimamia iwasili kwa kamati siku tatu kabla ya kikao husika."

"Hii inawapa wajumbe nafasi ya kusoma nyaraka kuzielewa, kutafuta ufafanuzi zaidi ili tutendee haki bunge lililotupa wadhifa huu wa kusimamia fedha za umma kwa hiyo tumewarudisha,"alisema.

Alisema Ofisa Masuuli ambaye ni Katibu Mkuu wa Ujenzi alizuia kuwasilishwa kwa nyaraka hizo kwa kamati akidai kuwa zina marekebisho.

"Kutokana na kutaka ile document ibebe maudhui aliyotaka Ofisi ya CAG ikaona basi tungoje maana Ofisa Masuuli ndio kasema hili na lile, kusema kweli aliyechelewesha kazi hii ni Katibu Mkuu wa Ujenzi maana CAG asingemkatalia kuwasilisha hayo marekebisho na ndio mwajibikaji mkuu katika kamati hii na ndio anayejibu hoja za bunge,"alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema kwenye utekelezaji wa majukumu kamati huzingatia baadhi ya sheria na nyaraka muhimu ikiwamo kanuni za bunge.

"Kanuni zinaelekeza taarifa zote zinazokuja kwenye kamati hii zinapaswa zifike katika kipindi kisichopungua siku tatu kabla, taarifa zao tumepokea asubuhi hii inaonesha kwamba wamelidharau bunge, hatuwezi kuendelea kuhoji kwa kudharau bunge,"alisema.

Aidha, alisema kuna sheria ambazo zinazingatiwa ambayo ni Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ambayo inalipa Bunge mamlaka ya kuwa na kamati hiyo kama chombo cha usimamizi wa fedha za serikali.

"Kuna Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2004 inatoa mamlaka kwenye Bunge kuhakikisha kwamba linasimamia fedha zote ipasavyo, pia ukichukua Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2008 lakini kuna Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sheria ya Bajeti inataka kila fedha ya umma inayotolewa lazima ipate idhini ya Bunge."

"Na sisi tumejiridhisha kabisa kwamba katika kipindi hichi cha mahesabu yaliyoishia Juni 30, 2020 wenzetu TANROADS wametumia fedha hizo Sh. bilioni 616.3 bila idhini ya Bunge na ni matumizi makubwa kinyume cha sheria na taratibu, miongozo na kanuni, tumeona kwamba Bunge linakuwa limedharaulika,"alisema.

Hasunga alisema kamati hiyo inataka maelezo ya kina ya kimaandishi ili kuangalia hatua zitakazochukuliwa na Bunge dhidi waliokiuka sheria za bunge.

Alisema taarifa za TANROADS zimeonekana zina mapungufu mengi ambayo yanayohitaji vielelezo vya kina ili kamati ifanyie kazi.

"Pia usimamizi wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara ambayo imetekelezwa katika maeneo mengi hawakusimamia ipasavyo, mingine inachelewa wanasaini mikataba halafu watekelezaji hawaanzi kutekeleza na kusababisha athari kubwa ambapo serikali hulipa fedha zaidi kuliko zilizokuwa kwenye mikataba, usimamizi wa mikataba sio mzuri kwa TANROADS,"alisema.

Alisema uchambuzi wa hoja hizo unatakiwa kufanyika baada ya kupata majibu ya kina na wanatakiwa kuwasilisha nyaraka hizo kesho kabla ya saa tisa na nusu alasiri.

Awali, akijitetea sababu ya kuchelewa kuwasilisha kwa nyaraka hizo, Katibu Mkuu anayeshughulikia Ujenzi, Mhandisi Joseph Malongo, alisema ni kutokana na kuwa na majukumu mengine ya kitaifa yeye na msaidizi wake ambaye ni Naibu Katibu Mkuu na kuomba radhi kwa kamati hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Uamuzi kesi ndogo ya Freeman Mbowe kesho

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi inatarajia kutoa uamuzi wa kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi ya ugaidi inayomkabili, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe (pichani) na wenzake watatu kesho.

Mahakama itatoa uamuzi kama mshtakiwa wa pili Adam Kasekwa aliteswa kabla na wakati akitoa maelezo ya onyo na kama maelezo hayo yalichukuliwa ndani ya saa nne ama la.

Uamuzi huo ulitarajiwa kutolewa leo lakini yametokea mabadiliko kwa sababu ni siku ya mapumziko na sasa utatolewa kesho, hatua hiyo imefikiwa baada ya Mahakama hiyo mbele ya Jaji Kiongozi, Mustapha Siyani kumaliza kusikiliza ushahidi wa mashahidi watatu kwa upande wa Jamhuri na watatu kwa upande wa utetezi.



Septemba 10, mwaka huu, Mbowe, Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire, walisomewa mashtaka na walikana kula njama kufanya ugaidi ikiwamo kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Shahidi wa kwanza katika kesi ya msingi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi, Kinondoni, Kamishna wa Polisi Msaidizi, Ramadhan Kingai alitoa ushahidi na katika ushahidi wake alidai kumsikia Luteni Denis Urio, akisema mbele ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz kwamba kuna kundi la kihalifu linaandaliwa na Freeman Mbowe na wanataka kufanya vitendo vya kigaidi.

ACP Kingai alipotaka kutoa maelezo ya onyo ya Kasekwa kama kielelezo, Wakili Peter Kibatala alipinga kupokelewa kwa madai mteja wao aliteswa kabla na wakati wa kuchukuliwa maelezo hayo na kwamba yalichukuliwa zaidi ya saa nne.

Upande wa utetezi uliomba iwapo kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi, mahakama ilikubali na mashahidi watatu upande wa mashtaka walitoa ushahidi wakionyesha kwamba mshtakiwa Kasekwa hakuteswa.

Mashahidi hao alikuwa ACP, Kingai, Inspekta Mahita Omari na Koplo Msemwa.

Upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi watatu ambao katika ushahidi wao walionyesha mshtakiwa Kasekwa aliteswa baada ya kukamatwa Moshi Agosti 5, mwaka 2020, alipofikishwa Kituo cha Polisi Moshi na alipofika Dar es Salaam Agosti 7, 2020 hakupigwa, lakini alipewa maneno yaliyomtia hofu akiwa Kituo cha Polisi Mbweni.

Mashahidi wa utetezi alikuwa Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na mke wa Kasekwa, lilian Kibona.

Mawakili wanaomtetea Mbowe ni Kibatala, Michael Mwangasa, Michael Rugina, Alex Masaba, Gaston Garubimbi, Deogratias Mahinyila, Hadija Aron, Selemani Matauka, Ferdnand Makole, Evaresta Kisanga, Marie Mushi na Jonathan Mndeme.

Mshtakiwa wa kwanza Halfani Bwire anawakilishwa na Wakili Nashon Nkungu na Jeremiah Mtobesya, mshtakiwa wa pili Adamu Kasekwa anawakilishwa na John Mallya na mshtakiwa wa tatu anawakilishwa na Dickson Matata.

Upande wa Jamhuri unawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, Nassoro Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin, Pius Hillar, Jenitreza Kitali, Abdallah Chavula na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige.




Wananchi wa Wilaya ya Longido wakimshangilia Rais Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa stendi mpya Longido mkoani Arusha katika ziara ya kikazi kutembelea, kukagua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi. **PICHA: IKULU**

# Waziri wa Ufaransa kutua nchini

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Kiuchumi wa Ufaransa, Franck Reister, ni miongoni mwa wageni watakaoingia nchini na ndege ya moja kwa moja ya Shirika la Air France inayotarajiwa kuwasili visiwani Zanzibar kutoka Paris.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Ufaransa nchini, kiongozi huyo atakuja Dar es Salaam kwa ziara ya kikazi ya siku moja na atakuwa na mazungumzo rasmi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Pia, atakutana na viongozi wengine wa ngazi za juu wa serikali pamoja na wafanyabiashara wa Tanzania na Ufaransa kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya kuendeleza ushirikiano na fursa za kibiashara.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara katika ziara ya siku mbili jijini Arusha, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema katika kukuza sekta ya utalii jitihada mbalimbali zimefanyika kufungua milango kwa watalii ikiwamo kuchukua tahadhari za corona.

Alisema kesho itatua ndege kutoka Paris, Ufaransa itakayotua Zanzibar na baadaye kwenda Dar es Salaam ikiwa na watalii wengi watakaotembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini na kwamba ni dalili za kufunguka kwa utalii na kukuza uchumi.

"Tunatarajia Tanzania tutapata watalii wengi kwasababu wenzetu wa Marekani na Ulaya watataka kwenda kutembea kupata hewa safi na ndiyo maana tulitayarisha filamu ya Royal Tour, waone vivutio vyetu, amani na mazingira ya nchi yetu na waje kwa wingi...na sasa tunamekubali chanjo na tumeondolewa katika orodha ya nchi zisizofaa kutembelewa duniani, tunasisitiza wafanyakazi sekta ya utalii wachache ili kuwaondoa hofu wageni," alifafanua Rais Samia.

**UBALOZI WA MAREKANI, FINLAND, NETHERLAND, NORWAY, HTT INFRACO, MEK ONE LTD & BUREAU VERITAS (T) LTD.**

**DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA: (LINARUDIWA)**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Marekani, Finland, Netherland na Norwegian.** watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani, Container na Magari tarehe 23 October, 2021 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set,Sofa bed, China base, Hutch, Chest drawer,Credenza, Dining table, Book case, Office desk, Chairs,File cabinet, Carpet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Freezer, Washer, Dryer, GYM m/c, A/c split units, Photocopy m/c, TV set, Computer set, Colour Printers, 2 units Container 20Fts Std, Generator KVA 33 Na vingine vingi.

**Magari,Genereta na Makontena yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Hiace Commuter Min Bus | 2KD Diesel Engine | **2014** | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon | VK56 Petrol Engine | 2013 | Umelipwa |
| 1 | Toyota ALPHARD Station Wagon | 2AZ Petrol Engine | 2005 | Umelipwa |
| 1 | Toyota NOAH Station Wagon | 1AZ Petrol Engine | 2005 | Haujalipwa |
| 1 | Land Rover Freelander Station Wagon | SAL Petrol Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 1 | Ford Ranger Double Cabin | WLTA Diesel Engine | 2009 | Haujalipwa |
| 3 | Mitsubish Canter P-up 3 Tons & 2 Tons | 4M51,4D36,4D33 Diesel | 94 -2000 | Umelipwa |
| 1 | Toyota DCM 3.5 Tons Pick up | 14B Diesel Engine | 1993 | Umelipwa |
| 3 | TATA 709 3.5 Ton & HCE 0.5 Ton P.up | Diesel Engine | 2011 | Umelipwa |
| 1 | Mitsubish Pajero Station Wagon | Petrol Engine | 2004 | Umelipwa |

**Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 20 mpaka 22 October, 2021, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.**

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Container atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 28 October, 2021 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Generator litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB na NBC** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu **atatakiwa lazima kuwa na bid namba** itakayopatikana getini.
7. **Kila mtu anayesiriki mnada ni lazima kuvaa Barakoa na kunawa na maji tiririka au Sanitaiza, Umbali wa mtu na mtu uzingatiwe.**

116520302

Kwa maelezo zaidi waone:
UNIVERSAL AUCTION CENTRE
E-mail: universalauction@hotmail.com
Insta:universalauctioncentre

PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA
Cell Number- +255 0754 284 926
Dar es salaam

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Fedha za UVIKO-19 utalii zionyeshe tija

**SEKTA** ya utalii imepata Sh. bilioni 90.2 za msaada wa kukabiliana na madhara ya UVIKO-19, kwa ajili ya kuleta mageuzi na kuboresha vivutio vilivyopo na kuongeza vipya ili kupata watalii wengi zaidi.

Athari za UVIKO-19 kwa sekta hiyo zimeonekana kwa sababu hutegemea wageni kutoka Ulaya, Marekani, China, India na kwingineko duniani. Ipo misimu yenye watalii wengi zaidi, kuna kipindi cha msimu wa kati na wastani kulingana na majira ya mwaka, lakini misimu ya utalii pia hutofautiana kutoka ukanda mmoja wa nchi hadi mwingine.

Kwa Tanzania miezi ya kazi nyingi ni Juni, Julai, Agosti, Septemba na Oktoba ambacho ni kipindi cha mafuriko ya watalii na fedha nyingi hupatikana wakati huo.

Hivyo Sh. bilioni 71.9 zitakazotolewa kuboresha sekta ya utalii ziwekezwe kwenye maeneo yaliyoathirika zaidi na UVIKO-19, katika Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka za Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), ile ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Tunashauri fedha hizi zitumiwe kukarabati barabara katika maeneo ya Hifadhi za Serengeti, Mkomazi, Tarangire, Nyerere, Kilimanjaro, Saadani na Gombe, eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, misitu 10 ya hifadhi ya mazingira asilia.

Eneo jingine la kutizamwa ni kuweka mfumo wa kielektroniki, kukarabati viwanja vya ndege nane katika hifadhi za taifa za Serengeti, Nyerere, Tarangire, Mkomazi, Saadani na Katavi. Pia kujenga malango matano ya kupokelea wageni katika maeneo ya Likuyu Sekamaganga na Msolwa katika Hifadhi za Nyerere, Mkomazi, Mapori ya Akiba ya Swagaswaga na Kijereshi.

Tunaikumbusha serikali kuwa kilio cha kuharibika kwa miundombinu kwenye baadhi ya maeneo yaliyohifadhiwa kimekuwapo hasa nyakati za mvua, kiasi cha watalii kukwama au kushindwa kuvifikia baadhi ya vivutio, hivyo ujio wa fedha hizi ni habari njema na wapenda utalii tunataka kuona mabadiliko.

Kama alivyosema Rais Samia Suluhu Hassan, wiki iliyopita wakati wa uzinduzi wa mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano ya UVIKO-19, alitaka fedha hizo kutumika kwa mujibu wa maelekezo huku akikemea uundaji wa kamati kama namna ya kujipatia fedha hizo.

Watakaopewa majukumu kwa kutumia fedha hizo wakumbuke kuwa wananchi wanachotaka ni kuona mabadiliko kwamba sekta ya utalii irudi kwenye mstari na kutoa ajira, kuwezesha mzunguko wa fedha na kuchagiza ukuaji wa maeneo mengine, kwa kuwa fedha hizi ni mkopo ambao kila Mtanzania anayeishi sasa na ambaye hajazaliwa atawajibika kuzilipa.

Tunaamini na hatutarajii kuona fedha hizo zinatumika kugharamia shughuli za uendeshaji zaidi badala ya kwenda kwenye miradi na ambayo itaonekana.

Maeneo kama ni barabara zitengenezwe kwa ubora na kupitika kwa kipindi chote cha mwaka na thamani halisi ya fedha ionekane. Tunawakumbusha waliopewa jukumu la kuisimamia sekta hiyo wakafanyakazi kwa uaminifu na uadilifu ili Watanzania watakapolipa deni wajue zimefanya kazi itakayowanufaisha wao na vizazi vijavyo.

Ni imani yetu kuimarika kwa sekta ya utalii na kuanza kuliingizia taifa fedha ni manufaa kwa kila Mtanzania kwa kuwa mbali na pato kuingia kwenye hazina na kugawanywa kwenye bajeti kuu, mzunguko wa fedha na ajira kwenye vivutio hivyo utainua maisha ya Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Mwandishi Wetu

## Isiishie kwenye juisi tu, TBS iangalie na tufaa

**BAADHI** ya bidhaa za matunda kama juisi inayotokana na matufaa au maepo imeelezwa kuwa si salama kwa wanywaji wake hatua inayosababisha vinywaji hivyo kuondolewa sokoni.

Juisi ya matufaa iliyokuwa inazalishwa na kuuzwa kwenye baadhi ya mataifa ya Kusini mwa Afrika imeondolewa sokoni ikielezwa kuwa ina sumu iitwayo 'patulin', inayotokana na fangasi wanaozalishwa ndani ya matufaa yaliyojeruhiwa au kuoza.

Kampuni inayozalisha matunda hayo inaeleza kuwa iwapo mteja atakunywa kinywaji hicho anaweza kupata madhara kama kutapika, kichefuchefu, kuvurugika tumbo na kuwa kwenye hatari za kiafya.

Ukweli ni kwamba licha ya Shirika la Viwango Nchini (TBS) kueleza kuwa Tanzania haina tatizo na uwapo wa juisi zenye sumu ya patulin inayotokana na fangasi, bado kuna haja ya kuangalia matufaa yanayouzwa sehemu mbalimbali nchini.

Kwa mfano matunda hayo yamesambaa kila mkoa hapa Tanzania. Yanauzwa karibu kila mahali na pengine ni kama njugu.

Wajasiriamali wanayauza pembeni ya barabara kubwa, lakini yamejaa kwenye vituo vingi vya mabasi vya mikoani au vya ndani ya mikoa. Yanapatikana kuanzia Mbezi hadi Tunduma mkoani Mbeya.

Na si hivyo tu, kwa ujumla ni tunda linalouzwa muda wote hapa nchini na linalopatikana misimu yote iwe kiangazi au masika.

Kutokana na kugundua kuwepo tatizo kwenye juisi za matufaa ni vyema serikali kuchukua hatua na kukagua na kufahamu hali halisi ya matunda hayo.

Ni vyema kuyaangalia matufaa hayo yanatoka wapi? Yanaingiaje nchini kama taarifa hizo hazipo. Yanahifadhiwa na dawa gani na je muda wake wa kuishi ni miezi mingapi yanapofikishwa sokoni ?

NI kwa sababu mengi inavyoelekea wanaoyanunua hawafuatilii taarifa za muda wa matumizi yake.

Mamlaka ya TBS ina jukumu la kuchunguza na kufahamu kwa undani matunda hayo ambayo wengi wanakula hata bila kuyasafisha na kuwapa wananchi taarifa ili kulinda afya zao.

Kuna maswali mengi yanayoibuka kuhusu matufaa au maepo yanayouzwa mitaani hasa kuhusu suala la uhifadhi wake, licha ya kupatikana kila mahali watu wanafahamu yanahifadhiwa wapi na kwa namna gani? Je, wauzaji wanazingatia utaalamu wa kuyatunza?

Maepo ni chakula ni vyema kuyakagua na kufahamu hali ya afya yake ili yasiwadhuru walaji, lakini kufuatilia yanakotoka na kuangalia viwango maana katika ushindani wa kibiashara mengi yanaweza kufanyika na kusababisha athari ambazo hazikutegemewa.

Tanzania ni eneo ambalo tatizo la njia za panya linavuruga mtiririko wa biashara hasa kwenye kuingiza bidhaa za vyakula kama mafuta , matunda na ndege kama kuku, mayai na vifaranga.

Kilichotokea kwenye juisi za epo zinazouzwa kwenye soko la Kusini mwa Africa (COMESA), kisiachwe kikapita bila kukagua maepo yanayoliwa na mamilioni ya Watanzania kila siku.

Ufuatiliaji unahitajika kwa sababu inawezekana wapo wafanyabiashara wanaouza na kuyaingiza matunda hayo nchini kwa njia wanazoziua wenyewe.

Licha ya matunda hayo kuuzwa kwa bei ya juu, kuna mengine yanayouzwa baada ya bei kupunguzwa na hata kufikia nusu ya gharama, hayo hutokea pale baadhi ya matunda hayo yanapoanza kuharibika kama kusinyaa na kuwa na vidonda.

Suala hilo lisichukuliwe kwa wepesi ni vyema kuchunguza na kuhakiki ubora ili kuwapa wananchi matunda bora kulinda afya zao na kwa kuzingatia kuwa ni heri kukinga kuliko kuponya.

Ni wakati pia wananchi nao kuwa makini kwa sababu waliokunywa juisi za epo kwenye soko la COMESA ambalo Tanzania si mwanachama wakapata madhara walitoa ripoti, hivyo hata wanaokula matunda hayo wanapoona kuna tatizo wasiche kuwapa maelezo wataalamu wa kufuatilia viwango na afya za walaji ili kurahisi kazi ya ufuatiliaji.

## Waitwa kupata msaada kisheria

Na Mary Geofrey

WANANCHI wa mkoa wa Dodoma na mikoa jirani wametakiwa kushiriki katika maonyesho ya Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI) ili kupata maarifa mbalimbali ikiwamo msaada wa kisheria.

Maonyesho hayo yatakayoshirikisha asasi zaidi ya 209 yanayotarajiwa kuanza Oktoba 23 hadi 28 mwaka huu na yatazinduliwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya wiki hiyo ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mkuu wa Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala, alisema maonyesho hayo yatakuwa fursa nzuri ya kushirikiana kati ya asasi za kiraia na serikali

"Wananchi watapata fursa ya kuonana na wataalamu mbalimbali wakiwamo wa kisheria ili kutatuliwa matatizo yao na kupatiwa msaada wa kisheria na hata fursa za kiuchumi kutoka kwa wachumi watakaoshiriki," alisema Lulu.

Alisema wiki hiyo itaenda sambamba na maonyesho na utoaji wa tuzo kwa asasi mbalimbali zilizofanya vizuri.

Alisema kauli mbiu katika maonyesho hayo inasema 'Azaki na Maendeleo' ikiwa na lengo la kuhakikisha mchango wa maendeleo ya Azaki unatambulika na kuwezesha maendeleo ya nchi.

Naye Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alitaja aina ya tuzo zitakazotolewa kuwa ni kwa asasi zilizofanya vizuri katika kutatua migogoro, zilizotetea haki za walemavu na haki zao, athari za UVIKO-19 na ushirikishaji jamii.

"Mashirikiano makubwa tunayoyapata kutoka serikalini yametuwezesha kama asasi kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii," alisema Anna.

Aliiomba serikali kuendelea kutoa ushirikiano zaidi kwa asasi hizo kwa ajili ya ustawi wa wananchi wake.

"Tunaomba wananchi washiriki kikamilifu katika maonyesho haya kwa sababu tutatoa msaada wa masuala mbalimbali. Wiki nzima hii iwe sherehe kwetu ya kushirikiana na jamii katika masuala mbalimbali yanayoendeshwa na Azaki hizi, " alisema Anna.

Naye Mtendaji Mkuu wa Foundation for Civil Society (FSC), Francis Kiwanga, alisema wakati wa maonyesho hayo wadau watapata fursa ya kufanya majadiliano na kuandaa maazimio ya kupeleka serikalini kwa ajili ya maboresho ya mpango mkakati wa maendeleo ya miaka mitano.

Alisema watatoa maoni na mapendekezo kwa mambo ambayo yataonekana hayapo katika mkakati huo.

# Faru kurejeshwa Hifadhi ya Mikumi

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

HIFADHI ya Taifa ya Mikumi iliyopo wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, inafanya utafiti wa faru ili kurudishwa katika hifadhi hiyo lengo kufikia wanyama watano wakubwa maarufu duniani.

Hatua hiyo itawezesha kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Mathew Mombo, alisema kwa sasa wanyama maarufu waliopo ni tembo, nyati, simba na chui ambao wamekuwa kivutio cha wageni wanaofika kutembelea hifadhi hiyo.

Alisema kuwa historia inaonyesha awali faru walikuwapo katika hifadhi hiyo miaka ya nyuma, hivyo wameamua kufanya utafiti ili kuona uwezekana wa mnyama huyo kurudishwa katika maeneo hayo.

"Sisi kama hifadhi tumeona umuhimu wa kufanya utafiti mbalimbali wa kuhakikisha tunamrejesha faru na hapa tutaweza kuitanga hifadhi zaidi na wageni wetu kuona wanyama wote watano," alisema kamishna huyo msaidizi.

Alisema kuwa kuwepo kwa faru kutaweza kuitangaza Hifadhi ya Mikumu zaidi na hivyo kuongeza idadi ya watalii kutokana na kupatikana kwa wanyama wote maarufu wakubwa.

Mombo, alisema faru atakaporejeshwa katika hifadhi hiyo atajengewa uzio maalumu kwa ajili kuzoea mazingira yaliyopo na baadaye ataachiwa.

Ofisa Mwandamizi na Mkuu wa Kitengo cha Utalii katika Hifadhi hiyo, Happiness Kiemi, alisema katika baadhi ya hifadhi ikiwamo Serengeti na Mkomazi wanyama maarufu watano wanapatikana hivyo ni vyema wageni wanaotembelea nao wakapata fursa ya kumwona faru anapokuwa Hifadhi ya Mikumi.

"Kwa sababu miaka ya nyuma Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ilikuwa ni moja kati ya maeneo yaliyokuwa na faru ambaye ni mnyama wa tano kukamisha idadi ya wanyama wakubwa watano, hivyo kwa sababu ilikuwa fursa hiyo basi itakuwa sio mbaya tukianzisha mchakato wa kukamilisha ili kufikia idadi ya wanyama hao watano," alisema.

Naye Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Idara ya Sheria na Ulinzi Mkakati, Greyson Maro, alisema hifadhi imeimarisha mipaka na kuwa salama na hakuna mtu anayeingia katika hifadhi au kufanya shughuli zozote kwenye mipaka bila kuwa na kibali ili kuhakikisha wanyama wote wanakuwa salama.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam, Jokate Mwegelo, akikabidhi msaada wa rangi zenye thamani ya Sh. milioni 15 zilizotolewa na Kampuni ya Coral Paints kwa Shule ya Msingi Kizinga iliyoko Mbagala Kizuiani katika kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kuboresha mazingira ya kufundishia. Kulia ni Mkuu wa Masoko wa kampuni hiyo, Adam Kefa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kikwazo kingine makazi mapya Magomeni Kota

Na Christina Mwakangale

WAKAZI wa Magomeni Kota mkoani Dar es Salaam wameshindwa kuhamia kwenye makazi mapya kutokana na kutokamilika kwa ufungwaji wa Luku, huku zikipatikana 100 kati ya 644 zinazohitajika kwenye kila kaya.

Mwenyekiti wa wakazi wa Magomeni Kota, George Abel, akizungumza na Nipashe jana, baada ya wakazi hao kufanya mkutano wao juzi kujadili suala hilo, alisema pamoja na kuahidiwa kuhamia kwenye makazi hayo mwezi huu, wamekuwa wakipokea majibu tofauti kila wanapofuatilia suala hilo.

Alisema walichokibaini ni kwamba mita za luku ndio zinazokwamisha wakazi hao kuhamia mapema, na kwamba mita zilizolipiwa TANESCO ni 106, huku zikihitajika zaidi ya 600 kulingana na idadi ya kaya, kutokana na kila familia kutakiwa kuwa na Luku yake.

"Ujenzi umekamilika, ila changamoto ni umeme, TANESCO mmoja wetu alifuatilia na ikabainika mita zilizolipiwa na TBA (Wakala wa Majengo) ni 106, hivyo zaidi ya 500 hazijalipiwa," alisema George.

Alisema wanaiomba serikali kufuatilia suala la wao kuhamia makazi hayo, kutokana na sintofahamu wanayoipata hivi sasa.

Mtendaji Mkuu waTBA, Daud Kondoro, akizingumza na Nipashe jana kuhusu suala hilo, alisema yupo safarini na kwamba atalizungumzia suala hilo, atakaporejea.

Septemba, mwaka huu, aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Leonard Chamuriho, aliwahakikishia wakazi hao 644 kwamba watahamia kwenye makazi mapya, Oktoba mwaka huu.

Alisema wakazi hao watakaa bila kutolipa kodi kwa miaka mitano kama walivyoahidiwa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, akisema kwamba makazi hayo yamekamilika kwa asilimia 99 na kilichobaki ni kufunga umeme.

Aidha, Kaimu Mkuu wa TBA, Said Mdeme alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 99, na kwamba kabla ya wakazi hao kuingia katika vyumba hizo TBA itatoa semina elekezi juu ya namna ya kuishi katika majengo hayo.

# Watumishi 18,300 wahamia Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira, Kazi na watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amesema watumishi wa umma 18,300 wamehamia Dodoma, huku zaidi ya Sh. bilioni tisa zilizokuwa zikitumika kupanga majengo Dar es Salaam zikiokolewa.

Mhagama aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya kusaini mkataba wa ujenzi wa majengo mawili ya Ofisi ya Waziri Mkuu awamu ya pili utakaofanywa na Mkandarasi kutoka Suma JKT na Mshauri elekezi ni Chuo Kikuu cha Ardhi kwa gharama ya Sh. bilioni 42.7.

Alisema tangu serikali ilivyotangaza azma ya kuhamishia shughuli zake Dodoma, Septemba 2016 hadi kufikia Juni mwaka 2021, watumishi hao wamehamia na Sh. bilioni 655.8 zimetumika kwa ajili ya kuhamisha watumishi, kutengeneza miundombinu ikiwamo kujenga majengo 23 ya wizara awamu ya kwanza.

Alisema hatua hiyo ya serikali imeokoa zaidi ya Sh. bilioni tisa kwa kuacha kupanga ofisi kadhaa za serikali katika majengo yaliyopo Dar es Salaam.

"Kabla hatujasema thamani ya uokoaji wa fedha kwenye maeneo mengine, upangaji wa ofisi na shughuli nyingine Dar es Salaam, tayari fedha hizo ziliokolewa kwasababu hapa Dodoma ofisi zinazotumika ni za serikali na nyingi mmeona tulijipanga vizuri, majengo yanayomilikiwa na taasisi za serikali tuliendelea kuyatumia," alisema.

Aliongeza "Rais Samia alivyoingia madarakani aliridhia mpango mkakati wa ujenzi wa Mji wa Serikali awamu ya Pili, tulifanya awamu ya kwanza tukajenga majengo haya ilikuwa ni lazima kikosi kazi chetu kilete mapendekezo ya mpango mkakati wa ujenzi wa awamu ya pili wa Mji wa Serikali."

Alibainisha kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwasilisha mpango huo kwa Rais Samia na kuridhia ujenzi huo kwa awamu ya pili na utekelezaji wa bajeti yake Sh. bilioni 600.84.

"Desemba mwaka huu Waziri Mkuu atafanya kazi kubwa sana ya kuzindua kazi hii kubwa kwa ujumla wake, mpango kazi huu umegawanya kazi ya ujenzi wa ofisi za majengo haya ya serikali kwa awamu mbili, kwa bajeti ya mwaka 2021/22, Rais ameridhia serikali kwenye bajeti yake itoe Sh. bilioni 300 za kutekeleza kazi hii kwa wizara zote na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, fedha itagawanywa mara mbili yaani ya kujenga majengo ya serikali na kutakuwa na fedha ya kutekeleza uwapo wa huduma za miundombinu zinazofanana na hadhi ya mji tunaokwenda kuujenga," alisema.

Alisema tayari wizara zingine zimeshasaini mikataba ya ujenzi na zingine zinakamilisha taratibu za manunuzi.

"Ofisi ya Waziri Mkuu itajenga majengo mawili ya kisasa na kila jengo lina vionjo vya tofauti na yataanzia ghorofa sita hadi 11, hakutakuwa na jengo lenye ghorofa tano kushuka chini, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tutakuwa na jengo la masuala ya uratibu wa shughuli za serikali lenye thamani ya Sh. bilioni 23.5 na tutakuwa na ofisi ya kazi, ajira na watu wenye ulemavu lenye thamani ya Sh. bilioni 19.2," alisema.

Kuhusu ujenzi wa ofisi hiyo, Mhagama alionya yasifanyike makosa yoyote yatakayokwenda kinyume na mwongozo wa ujenzi huo (BOQ) na kusisitiza thamani ya fedha isimamiwe ipasavyo.

Naye Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Tixon Nzunda, alisema ujenzi huo unafanyika kwa miezi 16.

Aidha, alisema kati ya wizara 18 kati ya 24 zimekamilisha mchakato wa manunuzi na tatu zipo kwenye mchakato wa mwisho.



Chifu Kingalu Mwanabanzi (mwenye kanzu), akiwa katika sherehe za kimila na washiriki wengine wa tambiko lililodumu kwa siku kadhaa, liliwakutanisha watu mbalimbali ambalo hufanyika mara moja kila mwaka katika makazi yake, yaliyoko kijiji cha Kinole mkoani Morogoro. **PICHA: ADELADIUS MAKWEGA**

# Wataka amani, umoja kuiendeleza Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Kalambo, Josephat Kandege, amesema umefika wakati kwa Bara la Afrika kuungana kutafuta suluhisho katika changamoto zinazolikabili ili kuleta amani, utulivu na ujumuishwaji wa raia ili kufikia malengo mbalimbali.

Kandege alisema hayo katika mkutano wa siku moja ulioandaliwa kwa ushirikiano wa Taasisi ya Amani na Mafunzo ya Migogoro (IPCS) na Taasisi ya Amani Tanzania (TPF) na kuhudhuriwa na washiriki wengine zaidi ya 100 wakiwamo wabunge, mawaziri wa zamani wa mambo ya nje na mabalozi, wataalamu, wasomi na vyama vya kiraia kutoka Tanzania, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) za Comoros, Ghana, Kenya, Msumbiji, Rwanda, Afrika Kusini na Uganda.

Kaulimbiu ya mkutano huo uliofanyika Dar es Salaam ilikuwa: "Utekelezaji wa Utafutaji wa Baada ya Covid-19: Je, Azimio la Sahara Linawezaje Kuchochea Utulivu na Ushirikiano wa Afrika?"

Katika mkutano huo, Kandege pia alisema raia katika nchi za Afrika wanapaswa kuhakikishiwa uhakika wa usalama wa chakula.

Mintarafu urithi wa Hati ya Casablanca na Hati ya Mababu wa Kiafrika wakiwamo Julius Nyerere (Tanzania) na Jomo Kenyatta (Kenya), washiriki walisisitiza umuhimu wa kukomesha aina zote za kujitenga na kuwa msimamo mkali ili kufanikisha vipaumbele vya Afrika kama utekelezaji wa Eneo la Biashara Huria la Afrika (AfCFTA) na Malengo ya Ajenda ya 2063.

Kwa mujibu wa Kandege, nchi za Afrika zinapaswa kukumbatia amani na kukuza biashara itakayohakikisha kunakuwa na idadi ya kutosha ya watu watakaoshiriki kukuza maisha na kukuza uchumi.

# Mume taabani madai ya kuchomwa kisu na mke

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Katunda, Manispaa ya Shinyanga, Simon Robert (43), amenusurika kifo baada ya kudaiwa kuchomwa kisu na mke wake Amina Hamis (32), kichwani, tumboni na kumsababishia majeraha.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, akitoa taarifa ya tukio kwa vyombo vya habari, alisema limetokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa saba.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi na kwamba wanandoa hao walianza kugombana baada ya kutoaminiana kwenye mahusiano yao na mwanamke huyo anadaiwa kuchukua kisu na kumchoma mwenzake kichwani na tumboni.

"Majeruhi amelazwa katika hospitali ya rufani mkoani Shinyanga akipatiwa matibabu na hali yake ni mbaya sababu alichomwa kisu sehemu mbaya za kichwani na tumboni," alisema Kyando.

Alisema Jeshi la Polisi limamshikilia mwanamke huyo kwa tuhuma za kumchoma mume wake na kisu na upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili.

Katika hatua nyingine kamanda alitoa wito kwa wanandoa wote, wajiepushe na masuala ya wivu wa kimapenzi, kama wana migogoro wakae wazungumze badala ya kujichukulia sheria mkononi.

## Soko lilivyofunga kiwanda cha chaki

**Na Dinna Maningo,** TARIME

KIWANDA cha chaki cha Victoria kinachomilikiwa na kampuni ya Arwa Investment kilichopo wilayani Tarime, Mkoa wa Mara kilichozinduliwa na aliyekuwa Makamu wa Rais (sasa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania), Samia Suluhu Hassan, kimefungwa baada ya kukosa soko la kuuza chaki mkoani humo.

Imeelezwa kuwa licha ya mkoa wa Mara kuwa na shule nyingi za msingi na sekondari na vyuo, lakini hazinunui chaki zinazozalishwa na kiwanda hicho badala yake zinazonunuliwa ni za kutoka mikoa mingine na nchi jirani ya Kenya.

Meneja uzalishaji wa kiwanda hicho, Magala Magembe, alisema kuwa kitendo cha bidhaa za ndani kutonunuliwa kunarudisha nyuma jitihada za wawekezaji wa ndani kwa kuwa watu wengi hawapendi kununua bidhaa za kwao na kukimbilia zile za nje.

"Kiwanda kilianza uzalishaji 2017, tuna miezi sita sasa kiwanda kimesimama uzalishaji kwa sababu chaki hazinunuliwi.

## Jamii Forums yatunuku washindi wa uandishi

**Na Mwandishi Wetu**

ASASI ya kiraia ya Jamii Forums imewazawadia fedha taslimu Sh. milioni 10, kompyuta mpakato na simu janja watumiaji wa mtandao wao 10 walioandika taarifa za kusaidia jamii kufanya mabadiliko.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa utoaji wa tunzo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Jamii Forums, Maxence Melo, alisema mashindano hayo yalianza Julai 14, mwaka huu na kufungwa Septemba 30, mwaka huu.

Alisema walipokea jumla ya wanachama 1,509 walishiriki na kuandika maandiko 1,539, lengo likiwa ni kuibua taarifa mpya na za kuisaidia jamii na serikali kufanya mabadiliko.

Katika mashindano hayo mshindi wa kwanza alikuwa Golder Mmari aliyejipatia Sh. milioni 5, wa pili ni Shija Masele aliyejipatia Sh. milioni 3 na wa tatu Elibariki Muna aliyejipatia Sh. milioni 2.

Washindi wengine ni Shabani Guo alijipatia kompyuta mpakato na Lyambogo Malembo alijipatia simu janja.

Aidha, Jamii Forums ilitoa tuzo ya heshima kwa Mzee Mohamed Said, mwanachama hai wa mtandao huo ambaye pamoja na mambo mengine amekuwa mstari wa mbele.

# Elimu kwa mlipakodi yawakuna wafanyabiashara wa Tunduma

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGEA

WAFANYABIASHARA wa mjini Songea mkoani Ruvuma wameipongeza Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa kufanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mkoani humo, wakisifu sasa kuwapo mabadiliko makubwa ndani ya mamlaka hiyo kulinganishwa na awali.

Wakizungumza wakati wa kampeni hiyo inayoendelea mkoani humo, wafanyabiashara hao walisema jana kuwa mbali na TRA kuwafikia na kuwapatia elimu ya kodi, kuna maboresho makubwa yamefanyika kwenye mifumo ya ulipaji kodi, suala ambalo limeondoa usumbufu kwa walipakodi.

"Mwanzoni mfanyabiashara alikuwa akichelewa kulipa kodi, TRA walikuwa wanakuja na kufunga maduka, lakini kwa sasa wameboresha mifumo yao kiasi kwamba tunakumbushwa kwa meseji kwenye simu zetu za mkononi na bado wanatufuata kutupatia elimu na kutukumbusha kulipa kodi kwa wakati, kwa kweli TRA wanastahili pongezi," alisema Chasiko Mhagama, mfanyabiashara wa mjini Songea.

Mfanyabiashara anayejishughulisha na ufuaji nguo kwa kutumia mashine, Advera Katabaruki, alieleza kuwa, kampeni ya elimu kwa mlipakodi imewasaidia kujua mambo mengi waliyokuwa hawayajui, akitolea mfano utunzaji wa kumbukumbu za biashara, matumizi sahihi ya mashine za EFD pamoja na umuhimu wa kulipa kodi.

"Kampeni hii ya elimu kwa mlipakodi imetufunza mambo mengi sana ambayo tulikuwa hatuyajui kama vile jinsi ya kutunza kumbukumbu zetu za biashara, kutoa risiti sahihi za EFD kwa wateja wetu na sisi kudai risiti tunapokwenda kununua bidhaa kwa wafanyabiashara wakubwa ikiwa ni pamoja na kutukumbusha kulipa kodi kwa wakati," alisema Katabaruki.

Mfanyabiashara wa vitambaa, Klasa Chengula, alisema amefurahia elimu aliyoipata na kuipongeza TRA kwa kubadilika tofauti na zamani walikuwa wanawaogopa maofisa wa mamlaka hiyo kwa kutokuwa na ukaribu na walipakodi wao.

"Kiukweli maofisa wa TRA wamejirekebisha sana tofauti na mara ya kwanza ilikuwa ukipigiwa simu unaitwa TRA tulikuwa tunapata mawazo kweli, lakini hivi sasa TRA haiogopeki na wamekuwa marafiki kiasi kwamba wamepita kutupa elimu nzuri ya kodi wala hatujajificha wala kufunga maduka," alisema Chengula.

Kampeni ya elimu kwa mlipakodi mkoani Ruvuma inaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali ya mkoani humo na walipakodi wanaelimishwa juu ya haki na wajibu wao, utunzaji wa kumbukumbu za biashara, umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati pamoja na kutoa risiti stahiki za EFD kila wanapouza bidhaa.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akieleza ubora wa dagaa wa Kigoma alipotembelea mwalo wa Katonga ulioko mkoani Kigoma kuangalia namna wavuvi wanavyokausha dagaa katika vichanja. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Kituo kupambana na ukatili kijinsia kujengwa

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Kiwohede, linatarajia kujenga kituo cha pamoja cha kuhudumia waathirika wa ukatili wa kijinsia chenye thamani ya Sh. milioni 95 katika Kata ya Bugarama, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga.

Hatua hiyo ni sehemu ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wadogo.

Shirika hilo linatekeleza mradi wa kuwezesha usawa wa kijinsia kwa wasichana balehe na kinamama vijana katika kata za Bugarama, Shilela na Kata ya Lunguya mkoani Shinyanga na Halmashauri ya Ikungi mkoani Singida kwa ufadhili wa UNFPA, UN-Women na KOICA.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Justa Mwaituka, aliyaeleza hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake ambapo alisema kuwa, mpaka mradi huo unakamilika mwakani watakuwa wameshawafikia na kuwahudumia wasichina balehe na wanawake vijana 450.

Alisema kuwa, kituo hicho kitakapokamilika kitakuwa na ofisi ya dawati la kijinsia, afya, ustawi wa jamii, Kamati ya Mtakuwwa ngazi ya kata pamoja na ofisi ya msaada wa kisheria ili linapokea kesi kuripotiwa katika kituo hicho iweze kupatiwa ufumbuzi kwa haraka zaidi.

Aidha Mwaituka alisema kuwa, fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho zimeshatikana na wanatarajia kuanza kazi hiyo muda wowote kuanzia sasa, na kwamba wanasubiri utaratibu na miongozo kutoka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halimashauri ya Masalala.

Pia alisema kuwa Kiwohede imeamua kujenga kituo hicho ili kitumike kwa ajili ya kutolea elimu ya madhara ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwenye maeneo ya mradi pamoja na kutumika kuwawezesha wanawake na watoto wa kike kiuchumi pamoja na kuwawezesha stadi mbalimbali za maisha.

Mmoja wa wakazi wa Bugarama, Kwandu Bundala, alisema kuwa, uwepo wa kituo hicho utasaidia kupunguza matukio ya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto kwenye maeneo yao kwa kuwa watakuwa na sehemu ya kukimbilia kwa ajili ya kupata msaada wa kisheria. Kwa upande wake, Paul Nkandi, alisema wanaofanyiwa vitendo vya kikatili wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 20 kutoka Kata ya Bugarama hadi makao makuu ya halmashauri kwenda kushtaki, na kwamba kitakapokamilika kituo hicho kitasaidia kuondoa adha hiyo.

Naye Ester Mabula, alisema kuna familia ambazo kinababa wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya kikatili na wake zao hasa kwa kunyimwa unyumba na kutelekezwa watoto hivyo nao watajitokeza kwa wingi kupata suluhu ya ndoa zao.

# ALAT yaahidi kutatua kero uhaba watumishi s/mitaa

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Tawala za Mikoa nchini (ALAT), Murshid Ngeze, ameahidi kutatua kero za uhaba wa watumishi kwa ngazi ya serikali za mitaa ili kusaidia usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Akizungumza na Nipashe kuhusu vipaumbele atakavyoshughulikia ili kuondoa matatizo yanayobainika wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Ngeze alisema katika maeneo yanayotekelezwa miradi ya wananchi hushindwa kukamilika kwa wakati na kuonekana kuwa na upungufu sababu ikiwa ni ukosefu wa watumishi katika eneo husika.

"Kuna baadhi ya halmashauri hazina watendaji wa vijiji ambao ndiyo wangeweza kusimamia miradi inayotekelezwa ngazi ya vijiji kwa kuwa hakuna wataalamu kuangalia na kutolea taarifa ya maendeleo," alisema Ngeze.

Alisema wasimamizi wanaokuwa wamepewa miradi hiyo siyo wataalamu wa jambo husika na hushindwa kufanya manunuzi sahihi ya vifaa.

"Nitolee mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba wahandisi waliokuwapo baada ya kuundwa kwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), walienda huko, hao ndiyo wangeweza kutembelea miradi ya miundombinu inayotekelezwa na kubaini upungufu unaotokea," alisema Ngeze.

Alisema hali hiyo inafanya shughuli nyingi katika sekta ya miundombinu katika halmashauri kutokidhi vigezo vya gharama inayokuwa imetolewa na serikali.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Hamad Chande, akizungumza katika moja ya mikutano ya Kamati ya Mawaziri 8 wa Wizara za Kisekta kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi mwishoni mwa wiki. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wakimbilia CCM iwasaidie kupata ardhi

**Na Renatus Masuguliko,**
CHATO

WAKAZI zaidi ya 1,000 wanaoishi maeneo jirani na msitu wa hifadhi katika Kijiji cha Nyalutefye wilayani Chato mkoani Geita, wamekiomba Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani humo kuwasaidia wasikamatwe na kuharibiwa mazao yao.

Wananchi hao wanakamatwa mara kwa mara kwa madai kwamba wanafanya shughuli zao katika maeneo ya msitu wa hifadhi.

Wakizungumzia hali hiyo, baadhi ya wawakilishi wa wananchi hao wamedai kwamba wamekuwa wakifukuzwa na kukamatwa huku mazao yao yakiharibiwa.

Walisema waliomba serikali kuwapatia eneo hilo ili walitumie kwa shughuli za kibinadamu ikiwamo kulima na kuishi lakini bado hawajajibiwa.

Mmoja wa wananchi hao, Sunani Juma, ni miongoni mwa wananchi wanaokumbwa na kadhia hiyo ya kukamatwa mara kwa mara katika maeneo hayo.

Alisema Wakala wa Huduma ya Misitu (TFS), wamekuwa wakifanya doria katika maeneo hayo na kuwakamata kwa madai ya kuingia sehemu zilizokatazwa.

Mwananchi mwingine, Simon Nyerere, alisema alianza kulima katika eneo hilo miaka mitano iliyopita baada ya serkali kufungua milango ya maeneo yaliyoharibiwa na shughuli za kibinadamu na kupoteza sifa ya kuendelea kuwa hifadhi.

Alisema aliyekuwa Diwani wa Buziku, Joseph Magoma, aliomba eneo hilo kupewa wananchi hao kwa ajili ya shughuli za kibinadamu, lakini hadi sasa majibu bado hayajatolewa.

Aliomba timu ya mawaziri 8 inayozunguka nchi nzima kutatua migogoro ya ardhi kufika kijijini kwao ili iwasaidie waweze kuendesha maisha yao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM wilayani Chato, Raphel Masambo, aliwaomba wananchi hao kuwa watulivu wakati suala lao likishughulikiwa kwani chama kinalitambua.

Aliwasisitiza wananchi hao kuendelea kulinda mazingira wakati wakisubiria matokeo ya kamati ya mawaziri hao waliotumwa kutembelea maeneo yeye migogoro kama yao.

Mwakilishi wa TFS Kanda ya Mwanza, Chrisman Joseph, alisema wananchi wenye uhitaji wa ardhi wanatakiwa kutuma maombi kwa mamlaka zinazohusika kabla hawajaanza kufanya shughuli yoyote ndani ya hifadhi.

# Vodacom yajizatiti ugawaji wa gawio

**Na Maulid Mmbaga**

KAMPUNI ya Vodacom imesema imeweka mikakati ya kupata faida ili kutoa gawio kwa wanahisa katika mwaka huu wa fedha.

Hatua hiyo inatokana na kupata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 30 mwaka uliopita. Kutokana na hasara hiyo, ilishindwa kutoa gawio kwa wanahisa wake.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa wanahisa uliofanyika jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Vodacom, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo, alisema hasara hiyo ilisababishwa na changamoto mbalimbali ikiwamo UVIKO-19.

Alisema kutoa gawio kwa kampuni ambazo zimeorodheshwa katika soko la hisa kwao ni kipaumbele, lakini moja ya vitu vilivyoikwamisha kampuni hiyo ni utaratibu wa kusajili laini kwa alama za vidole ambao ulipunguza wateja wa Vodacom zaidi ya milioni 2 na kusababisha kupata hasara kwa zaidi ya asilimia 5.7.

Alibainisha kuwa katika uwasilishaji, mapato ya huduma yaliyoripotiwa ni Sh. bilioni 966 ikiwa ni chini ya asilimia 5.7 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Viashiria vingine vilivyoripotiwa ni Sh. bilioni 356.8 katika mapato ya M-Pesa na Sh. bilioni 186.9 katika mapato ya data, yaliyoongezeka kwa asilimia 3.3.

"Tutafanya kila linalowezekana chini ya sheria ili mwaka huu wanahisa wapate gawio, hatuwezi kusema lazima kwa kuwa hatujui ya mbeleni, lakini tumeanza kuona ishara ya matumaini. Mtu kama alikuwa anatumia mashine mbili za kupumulia moja ikiondolewa unashukuru.

"Hakuna kampuni isiyopenda kutoa gawio, uamuzi wa kutotoa gawio ni jambo zito ambalo linamuuma kila mtu ukifikiwa watu hawalali kwakuwa ni kinyime na matarajio ya wanahisa, lakini wameridhia katika mkutano mkuu kwa kuwa imefanyika hivyo ili kampuni iendelee kustawi," alisema Jaji Mihayo.

Aidha, aliongeza kuwa wanahisa wameafiki agenda zote za mkutano mkuu ikiwamo ya kumwajiri Mkurugenzi Mtendaji Mpya, kuwaongezea muda baadhi ya watendaji na wamekubaliana kuwa ifikapo mwezi Novemba mwaka huu, wataangalia mwenendo wa biashara ya kampuni hiyo na taarifa itatolewa kwa wanahisa kwamba wanakwendaje.

Aidha, kuhusu tozo mpya zilizoanzishwa na serikali katika mwaka huu wa fedha ni mojawapo ya sababu nyingine iliyotikisa biashara, kwani watu wengi wamepunguza kutuma fedha kwa njia ya mtandao na badala yake wanatumia njia mbadala.

"Kusema kweli tozo zimeathiri biashara baadhi ya watu wameacha kutuma fedha kwa njia ya mtandao nikiwemo mimi mwenyewe ila tunashukuru baada ya serikali kuingilia kati na kupunguza kama asilimia 30 lakini tunaangalia mahesabu bado haijaleta utofauti mkubwa.

"Tunaishukuru serikali kwa kuona kuwa bado iko tayari kutusikiliza kwani imetuambia tuendelee kupeleka maoni yatakayosaidia kuona ni namna gani bora ya kuifanyia marekebisho sheria hiyo," alisema Jaji Mihayo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, ambaye anamaliza muda wake mwishoni mwa mwezi huu, Hisham Hendi alishukuru uongozi pamoja na wadau mbalimbali wa kampuni hiyo alioshirikiana nao katika kipindi chake chote huku akiwatakia utendaji kazi mwema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 19, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 14

## Ndivyo chama kitakavyolitoa gizani taifa vichwa vikubwa, mgongo wazi



Ukurasa 12

## UDSM NA AJIRA ZA WAHITIMU
Mkoa kwa mkoa kuwaondoa gizani, changamoto zinavyogeuzwa fursa

SAYANSI

NA FAUSTINE FELICIANE

# Ubaridi wa 'la nina' na joto kali vinavyokimbiza mvua za vuli


Ukame na vumbi ni shida inayoikumba mikoa mingi nchini kutokana na kuwapo upepo mkali mwaka huu, pamoja na kuchelewa mvua za vuli. **PICHA: MTANDAO**

KWA baadhi ya mikoa ya Bara na Visiwani hiki ndicho kipindi cha mvua za vuli kinachoanza mara nyingi Oktoba hadi Desemba, lakini inavyoelekea mwaka huu ukame unanukia.

Viashiria vinavyotolewa na Mamlaka Hali ya Hewa (TMA) mwezi mwaka huu, vinawataka wananchi kuchukua tahadhari.

TMA inasema viashiria vinavyoonekana kwa asilimia kubwa vinaashiria kuwa mvua zitakuwa za chini ya wastani na maeneo mengi yatakuwa na ukame ikitaja mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara na kaskazini ya Kigoma wilaya za Kibondo na Kakonko.

Aidha, ukame unanukia katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Pwani ya Kaskazini, kisiwa cha Mafia, Unguja, Pemba, Tanga na Dar e Salaam, anasema Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri wa Hali ya Hewa (TMA), Dk. Hamza Kabelwa.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kutoa utabiri huo mwezi uliopita, anawahimiza wakazi wa mikoa itakayoathirika kuchukua tahadhari na kufuata ushauri wa wataalamu kulingana na madhara ya ukame katika maeneo yao.

"Huu ni utabiri ambao TMA tumefuatilia vyanzo vyetu na kuona viashiria vya kuwapo kwa ukame, kama wataalamu tunatoa ushauri wetu, lakini kuna ushauri wa sekta mbalimbali kwenda kwa wananchi," anasema Kabelwa.

Anaungwa mkono na Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti na Matumizi ya Hali ya Hewa wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, anayezikumbusha kamati za maafa za mikoa hiyo kuchukua tahadhari za athari zinazotarajiwa kutokea.

"Utabiri huu kabla ya kuutoa tulikutana na wadau wa sekta mbalimbali wakiwamo wanaoshughulikia maafa lengo ni kuwapa ushauri ambao watautumia na kuwapa Watanzania katika maeneo ambayo tunaona kutakuwa na mvua ndogo za kufika mpaka chini ya wastani," anasema Dk. Chang'a.

Akizungumzia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa ambayo TMA imeona kabla ya kutoa utabiri, Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri, Dk. Kabelwa anasema katika mifumo hiyo kumeonekana uwezekano wa kuwapo kwa joto la bahari la wastani katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi na joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa eneo la mashariki mwa bahari hiyo.

Hali hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevu kuelekea katika maeneo ya pwani ya Tanzania.

Aidha, joto la bahari la juu ya kiwango cha wastani hadi juu ya wastani linatarajiwa katika bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola, hali inayotarajiwa kupunguza msukumo wa upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuingia Tanzania.

"Eneo la kati la kitropikali katika Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa na joto la chini ya wastani, linaloashiria kuwepo kwa 'La Nina' (ubaridi mkali baharini), utakaochangia upungufu wa mvua katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka," anasema Kabelwa.

"Sasa viashiria hivi vinaonyesha kwetu hatutakuwa na mvua au zitakuwa za wastani mpaka chini ya wastani na kwa baadhi ya maeneo yatakuwa na vipindi vikubwa vya ukame," anaongezea Dk. Kabelwa.

**USHAURI KWA UMMA**

Dokta Kabelwa anasema kuwapo kwa ukame kutaathiri sekta mbalimbali zikiwa kilimo, nishati na maji, mifugo na uvuvi, afya na biashara.

"Kwa mfano kwenye kilimo tunategemea maeneo mengi yatakuwa makame na ardhi kukosa unyevu, hivyo kutakuwa na shida kwenye kilimo, hapa tumeshauri wakulima walime mazao yanayostahimili ukame na kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo.

"Lakini pia kwenye sekta ya afya kutokana na kukosekana kwa maji safi na salama kuna uwezekano wa kutokea mlipuko wa magonjwa, hapa tunawashauri watalaam wa afya kuchukua tahadhari kupunguza athari hasi ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kuchemsha au kutibu maji kabla ya kuyatumia, kunywa maji ya kutosha kuepuka upungufu wa maji mwilini," anasema Dk. Kabelwa.

Kwenye nishati, anakumbusha kuwapo na upungufu wa maji kwenye vyanzo vya nishati hususani mabwawa ya kuzalisha umeme hivyo kunaweza kukatokea uhaba kwenye mitambo inayotegemea maji.

"Mwaka 2005 kulitokea ukame ndivyo tunavyotarajia mwaka huu, kulikuwa na uhaba wa nishati pia hivyo sekta hii inapaswa kuchukua tahadhari mapema kuepusha matatizo" anasema Dk. Kabelwa.

Anaeleza kuwa kamati za maafa katika kila mkoa kama zilivyopewa nguvu na sheria mpya, zinapaswa kuanza kuchukua tahadhari mapema na kuwashauri wananchi wa mikoa itakayoathirika njia sahihi za kukabiliana na ukame unaotazamiwa.

Sheria mpya ya maafa imewapa mamlaka Makatibu Tawala wa Mikoa kuratibu na kushughulikia maafa yote yanayotokea.

Kuonyesha utabiri wa TMA umewafikia viongozi mikoani, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera ambao ni miongoni mwa maeneo yanayotarajiwa kuwa na mvua za wastani mpaka chini ya wastani, Profesa Faustine Kamuzora, anasema wameanza kuzifanyia kazi taarifa ya TM za uwezekano wa kutokea kwa ukame na kwamba ipo mikakati ambayo tumeiweka kama mkoa," anasema Profesa Kamuzora.

Vipindi hivyo vya mvua za vuli vinatarajiwa kuanza kwenye maeneo mengi yanayopata mvua hizo kuanzia wiki ya tatu ya Oktoba na kumalizika katikati ya Desemba.

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

### UDSM NA AJIRA ZA WAHITIMU

# Mkoa kwa mkoa kuwaondoa gizani, changamoto zinavyogeuzwa fursa




Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), wakiwa katika mahafali yao. **PICHA: MTANDAO.**

UPATIKANAJI ajira kwa wahitimu na vijana kwa ujumla ni changamoto inayozikabili karibu familia zote, watoto wamemaliza shule za msingi, vyuo vya kati na vikuu lakini hawana cha kufanya. Hawaajiriki wala hawawezi kujiajiri.

Licha ya kwamba ni shauku ya wanafunzi wa ngazi zote kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu kupata kazi baada ya kuhitimu masomo ili kuendesha maisha yao, uwezekano huo unazidi kupungua.

Ukosefu wa mafunzo na ujuzi stahiki kwa wahitimu unatajwa kuwa ni moja ya kikwazo kinachokwamisha upatikanaji wa kazi baada ya kuhitimu.

Kutokana na hali hiyo serikali inazielekeza taasisi za elimu kubuni njia mbadala za kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira kwa kuandaa mafunzo kwa wahitimu ili yawe nyenzo ya kuwasaidia wahitimu kuajiriwa au kujiajiri.

Katika kutimiza azma hiyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeandaa mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu yenye kaulimbiu, "badili changamoto kuwa fursa" ili kuwajengea uwezo wahitimu kukabiliana na tatizo la kukosa ajira baada ya kuhitimu masomo yao vyuoni.

Mafunzo hayo ya ujasiriamali yameanza kutolewa kwa baadhi ya mikoa na kwa ujumla yataifikia mikoa 10 ya Bara na Zanzibar na wanufaika ni vijana wahitimu wa Dar es Salaam, Morogoro, Mtwara, Tanga, Dodoma, Kigoma, Mjini Magharibi, Geita, Kilimanjaro na Njombe.

Kila mkoa ukiwa na ratiba yake ya mafunzo na lengo kuu la kunolewa vijana hao ni kuwapatia uelewa, taarifa, maarifa, ujuzi na uwezo wa kuainisha fursa zinazowazunguka ili wazione na wazitumie fusa hizo ikiwa ni pamoja na kuanzisha biashara, kilimo, uvuvi, ubunifu, teknolojia na ufugaji ili kutoa ajira kwa wengine na hivyo kuboresha maisha ya jamii kwa ujumla.

Aidha, mafunzo hayo yana malengo mahususi kama vile, kujenga uwezo na tabia ya kutumia taaluma zao kutambua matatizo, changamoto na fursa za maendeleo kama za kibiashara.

Kukutana na kujifunza kutoka kwa wajasiriamali wazoefu wanaotoka kwenye sekta mbalimbali. Vilevile, kutengeneza mipango ya biashara ambayo itawasaidia kutafuta mitaji na pia kuwaunganisha na vijana wenye mawazo bora ya kijasiriamali na watoa huduma za kifedha, kiteknolojia na uatamizi.

Walengwa ni vijana wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu kuanzia diploma wenye nia ya kujiajiri na kukabiliana na changamoto za ukosefu wa ajira zilizo mbele yao.

Mafunzo hayo yatatolewa katika makundi ya watu wasiozidi 50 kwa darasa kila mkoa na watafunzwa bila kugharamia chochote, lakini kwa wahitimu kutoka mikoa ya mbali watajigharamia usafiri wa kwenda na kurudi pamoja na malazi.

Baadhi ya mikoa kama Dar es Salaam, Morogoro, Mtwara na Tanga mafunzo yalishaanza yakitarajiwa kumalizika Alhamisi wiki hii Oktoba 14.

Kuanzia wiki ijayo Oktoba 18 hadi 21 wahitimu wa mikoa ya Dodoma, Mjini Magharibi watafikiwa na mafunzo wakati awamu ya mwisho itaelekea Geita Oktoba 20 hadi 28 ikifuatiwa na Kilimanjaro na Njombe mafunzo yatakayokamilika mwisho wa mwezi wa Oktoba.

Kimsingi mkakati huu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu

> Mafunzo ya utengenezaji wa mipango ya biashara (business plan) ni muhimu kwa dunia ya sasa, kutokana na kuwapo kwa baadhi ya watu, mashirika na taasisi zinazohitaji kutengenezewa mipango ya biashara ili waweze kuiweka katika utekelezaji.

utawawezesha na kuwafanikisha katika kupambana na changamoto ya ajira na hatimaye kusaidia jitihada za nchi za kujiletea maendeleo.

Wahitimu watakapojengewa uwezo wa kujua namna bora ya kutumia taaluma zao na vipaji vyao katika kukamata fursa za kibiashara wapanue wigo wa ajira na hata kuajiri vijana wenzao.

Mafunzo ya utengenezaji wa mipango ya biashara (business plan) ni muhimu kwa dunia ya sasa, kutokana na kuwapo kwa baadhi ya watu, mashirika na taasisi zinazohitaji kutengenezewa mipango ya biashara ili waweze kuiweka katika utekelezaji.

Hivyo basi, kama wahitimu watapewa mafunzo na ujuzi wa namna bora ya utengenezaji wa mipango ya biashara, watapata soko la kuuza mipango hiyo na hatimaye kujiingizia fedha.

Ikumbukwe kuwa sekta binafsi ndiyo injini ya maendeleo ya uchumi wa nchi na kutokana na ufinyu wa nafasi za ajira serikalini, ni muhimu serikali kutekeleza mikakati ya kuiwezesha sekta binafsi hasa kuweka mazingira bora na rafiki ya ufanyaji biashara na shughuli za uwekezaji na hivyo kupanua soko la ajira kwa wahitimu na vijana wa Tanzania hasa hao waliofunzwa na wengine wengi.

Ni wakati muafaka sasa kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanyia kazi mapendekezo ya wadau mbalimbali kuhusu haja ya kuhuisha mitaala ya elimu ili kuwajengea uwezo wanafunzi kupata ujuzi na mafunzo wakiwa shuleni na vyuoni na si kusubiri mpaka wakihitimu.

Hili likifanyika, litapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ukosefu wa ajira kwa wahitimu na vijana. Kwa sasa mitaala inawaandaa wahitimu kusaka ajira badala ya kujiajiri wenyewe.

Ni vyema sasa wanafunzi wakafundishwa kilimo, sanaa, ufugaji, ujasiriamali, biashara, ufundi na ubunifu, wa aina mbalimbali wakiwa shuleni na vyuoni ili wanapohitimu wawe na ujuzi utakaowasaidia kujiajiri.

**Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali Dodoma.**

TEKNOLOJIA
NA MWANDISHI WETU, KIGOMA

# TARI inavyoibua michikichi bora kwa mafuta mengi

## ■ Ni kutumia mbegu 'jike dura' na 'dume pisifera'



Mratibu wa Michikichi wa TARI, Kuzenza Madili (kushoto), akifafanua hatua mbalimbali wanazozipitia kuandaa mbegu na miche ya tenera kwa Mkurugenzi wa Uhaulishaji wa Teknolojia na Uhusiano wa TARI, Dk. Juliana Mwakasendo (kulia). Katikati ni Dk. Filson Kagimbo, Mkurugenzi wa TARI Kihinga. **PICHA: TARI**

KATIKA kuliondoa taifa kwenye changamoto ya uhaba wa mafuta ya kula Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), imezalisha zaidi ya mbegu bora na chotara 7,200,000 za michikichi aina ya tenera.

TARI inaitaja tenera kuwa ni mbegu bora ya chotara iliyotafitiwa na kuzalishwa na TARI, kwa kutumia mbegu jike za kienyeji aina ya 'Dura' na mbegu ya kiume aina ya 'Pisifera' ambazo kwa kawaida hutoa mafuta kidogo ikilinganisha na mbegu chotara ya tenera.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha TARI-Kihinga kilichopo mkoani Kigoma, Dk. Filson Kagimbo, anasema katika mahojiano na Nipashe kuwa hadi sasa wametafiti na kuzalisha mbegu milioni 7.2.

Anasema kuwa endapo mbegu hizo zingeagizwa kutoka nje miche hiyo ingegharimu zaidi ya shilingi bilioni 16.

"Haya ni maendeleo makubwa katika kufanya utafiti na uzalishaji wa mbegu bora aina ya tenera kwa wakulima wetu. Jukumu letu kama tulivyoagizwa na serikali ni kuendelea kuzalisha kwa kasi na kuzigawa kwa wakulima kupitia halmashauri zao ili kila anayehitaji mbegu hizi apawe bure," anasema.

Mkurugenzi Kagimbo anasema kuwa kituo cha utafiti wa kilimo Kihinga kimesambaza mbegu hizo katika halmashauri zote Kigoma na pia katika halmashauri nyingine 11 katika mikoa mingine nchini.

"Huu ni mwanzo tu. Hatuishii hapa katika uzalishaji bali tumeongeza kasi ili kufikia uzalishaji wa mbegu milioni 10 kwa mwaka ambazo zitawafikia wakulima wote wanaoonyesha nia katika maeneo yote yenye hali ya hewa na rutuba ya kutosha kwa kilimo cha michikichi aina ya tenera.

Ili kuhakikisha uzalishaji endelevu wa zao hili Dk. Kagimbo anasema kituo cha utafiti wa kilimo Kihinga kimetoa mafunzo kwa maofisa ugani zaidi ya 124 kuhusu mbinu za kilimo bora cha zao hilo mkoani Kigoma.

Kadhalika, kituo hicho kimetoa mafunzo kama hayo ya kilimo bora cha michikichi kwa wakulima zaidi ya 1,200 na kazi ya utoaji mafunzo bado inaendelea kwa wakulima mbalimbali mkoani humo.

"Tumefanya mafunzo haya kwa makusudi kwa lengo la kuwawezesha wakulima na maofisa ugani waweze kuelewa mbinu na utaratibu wa kilimo bora cha zao la michikichi ili wakulima waweze kuongeza uzalishaji na pia waendeshe kilimo chenye tija mkoani Kigoma.

Dokta Kagimbo anafafanua kuwa tayari kituo chake kimewafikia wakulima zaidi ya 6,000 kupitia mafunzo mbalimbali kama vile maonyesho ya Nanenane, ya biashara, vyombo mbalimbali vya habari na ziara za watafiti mkoani humo.

Mbali na kutoa mafunzo kwa maofisa ugani na wakulima, TARI Kihinga imewafunza wanafunzi wa sekondari zaidi ya 90 na mpaka sasa kuna baadhi ya shule zimepanda michikichi na nyingine zina vitalu vya awali na vikubwa vya zao hilo katika maeneo yanayozunguka shule hizo.

"Kadhalika tunaendelea kutoa mafunzo haya kwa wasomi kama wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu. Kwa mfano mpaka sasa tumeshatoa mafunzo haya kwa wanafunzi wa vyuo zaidi ya 30 kutoka vyuo vikuu mbalimbali ambao wanaomba kufanya mafunzo kwa vitendo (field practical and formal training) hapa kituoni kwetu.

Anaongeza kuwa hivi sasa kuna kundi kubwa la wakulima ambao wanatuma maombi ya kupata mafunzo ya namna bora ya kulima mchikichi kutoka halmashauri mbalimbali mkoani Kigoma.

"Tunaishukuru sana serikali ya awamu ya sita kwa mkakati wa kuinua zao hili ili kukabiliana na uhaba wa mafuta. Kwa jitihada na mikakati tuliyonayo nina imani uhaba wa mafuta unaenda kupata majibu hivi karibuni," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Uhaulishaji wa Teknolojia na Mahusiano wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Dk. Juliana Mwakasendo, anasema ili kusaidia wakulima na wadau wengine kuzalisha kwa tija, TARI imefanikisha kazi ya kusambaza teknolojia mbalimbali kwa wakulima ambazo ni nzuri na tayari zimeshaanza kuzaa matunda.

Anazitaja teknolojia hizo kuwa ni pamoja na matumizi ya mbegu bora, utaalamu wa kilimo bora cha zao hilo la michikichi, usindikaji na namna ya kuongeza thamani.

"Tutaendelea kusambaza teknolojia hizi kupitia kituo chetu cha TARI Kihinga, kufanya semina na ziara kama hizi ili wakulima wetu waweze kuzalisha kwa tija.

Anasema lengo ni kuona wakulima wanalima kwa tija, lakini wanapata mafuta mengi ya kula na ya kuuza ili kuongeza kipato chao, pia kuchangia juhudi za kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kula nchini.

"Nawashauri wakulima wachukulie hili zao kama fursa ya kipekee, wafufue mashamba yao waanze kulima michikichi kwa sababu mbegu zinagawiwa bure, mafunzo yanatolewa bure. Gharama kubwa zimebebwa na serikali kupitia TARI kama vile mbegu bora na mafunzo ya kilimo bora," anasema.

Hapo awali wakulima walizoea kulima mbegu ya zamani aina ya dura ambayo uzalishaji wake wa mafuta ni mdogo. Kwa mfano dura hutoa tani 1.6 kwa hekari wakati mbegu mpya aina ya tenera inatoa mafuta tani tano kwa hekta.

Aidha, dura huchukua miaka mingi kukua na kuanza kutoa mafuta. Inakadiriwa kuwa mbegu hii huchukua miaka kati ya saba hadi 0 kuanza kutoa mafuta wakati mbegu mpya iliyoboreshwa aina ya tenera huchukua miaka mitatu tu kuanza kutoa mafuta.

Kwa mfano, miche aina ya tenera iliyopandwa ukiwamo ule uliopandwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Februari mwaka 2019, wakati anazindua zoezi la upandaji wa miche hiyo mkoani Kigoma tayari imeshaanza kutoa matunda na inakadiriwa kuwa itaanza kuvunwa kuanzia Desemba mwaka huu.

Kutokana na takwimu za miaka ya hivi karibuni, inakadiriwa kuwa matumizi ya mafuta nchini ni tani 570,000 ambazo kati ya hizo 365,000 zinaagizwa kutoka nje na zilizobakia 205,000 ndio zinazalishwa nchini.

Kiasi hicho cha mafuta kinachoagizwa kutoka ughaibuni kinaigharimu nchi zaidi ya Shilingi bilioni 444 kila mwaka.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Ndivyo chama kitakavyolitoa gizani taifa vichwa vikubwa, mgongo wazi

CHAMA cha Wazazi Wenye Watoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi (ASBAHT), kinaamini kuwa Watanzania wanahitaji elimu ili kuifahamu hali inayosababisha watoto kuzaliwa na ulemavu huo, ili jamii iwakubali na kuwafikisha kwenye huduma za kurekebisha hali zao.

Endepo wananchi wataelimishwa idadi kamili ya watoto wenye ulemavu huo itafahamika kwasababu ukosefu wa elimu ya mgongo wazi na kichwa kikubwa ni miongoni mwa sababu zinazowafanya wazazi na walezi waendelee kuwaficha.

ASBAHT inasema ukosefu wa elimu sahihi kuhusu chanzo chake unachangia baadhi ya wazazi kuwaficha watoto wenye tatizo hilo na kusababisha liendelee kuwapo badala ya kuchukua hatua za kulidhibiti.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mratibu wa ASBAHT, Hidaya Alawi, anasema chama kinajipanga kutoa elimu kwa jamii kuhusu chanzo cha tatizo na hatua za kuchukuliwa kulipunguza.

"Tangu chama kilipoanzishwa mwaka 2001, hatujawahi kupata takwimu za idadi ya watoto wenye tatizo hizo hilo, tunajua wale walioko katika hospitali mbalimbali wakipewa huduma, ambao ni zaidi ya 4,000," anasema Hidaya.

Aidha, anaeleza kuwa chama hicho kinataka kujua idadi ya wale waliopo majumbani ili kiwe na hesabu kamili ili nao waanzishiwe huduma za afya, kwa vile tunahitaji kuona kuwa wanaishi.



Mratibu wa Chama cha Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHT), Hidaya Alawi, akizungumza kwenye kikao cha chama hicho. **PICHA: SABATO KASIKA**

**UTOAJI ELIMU**

Anataja mikakati yao kuwa ni kushirikisha vyombo vya habari na madaktari katika kila hatua ya utoaji wa elimu na pia kuongeza matawi ya chama hicho, ili kufikisha mikoani kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa elimu.

"Tatizo ambalo tumegundua, ni ukosefu wa elimu sahihi kwa jamii ili kuliepuka kwani baadhi ya watu hudhani linatokana na mambo ya ushirikina na kusababia liendelee kuwapo badala ya kulidhibiti," anasema.

Baadhi ya watoto hufichwa majumbani na wengine kutishiwa maisha na wazazi, walezi au wanafamilia, na kwamba jambo hilo halikubaliki na ni kinyume na haki za binadamu.

"Zipo familia zimesambaratika baada ya kupata mtoto mwenye ulemavu huu, na waathirika wakubwa ni kinamama waliotelekezwa na wazazi wenza kwa kisingizio kuwa watoto wenye ulemavu huo ni mkosi katika familia," anasema.

Anasema, chama hicho kinaamini kuwa vyombo vya habari vina nguvu kubwa, na kwamba kitavitumia kutoa taarifa zake zirushwe mara kwa mara ili jamii ielewe chanzo cha tatizo na kuchukua hatua za kulikabili.

"Kuna changamoto kubwa hasa za ukosefu wa elimu sahihi kuhusu ulemavu huu kwa walio wengi. Hivyo kutumia vyombo vya habari itakuwa ni fursa kwa jamii kuelewa chanzo, dalili na tiba," anasema.

Kwenye suala la kuongeza matawi, anasema yatakuwa yanakwenda kwenye jamii na kutoa elimu na pia kupata idadi kamili ya watoto wenye tatizo hilo, ili chama kiwe na takwimu sahihi zitakazosaidia katika utoaji wa huduma za afya.

"Tutaanza kazi hiyo Januari mwaka ujao, ratiba itatolewa katika maadhimisho ya Siku ya Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi, yatakayofanyika Oktoba 25 mwaka huu jijini Dar es Salaam," anasema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii na Elimu ya Watu Wazima, Theresia Tarimo kutoka Taasisi ya Mifupa MOI, anasema, watoto wenye tatizo hilo wana haki ya kupata elimu kama walivyo wengine.

Anafafanua kuwa mtoto mwenye ulemavu wa aina hiyo akipata huduma mapema, anaweza kusoma na kufaulu vizuri na hata kuhitimu vidato, na kulitumikia taifa baadaye.

> "Mimi niko MOI, pia ninafanya kazi na ASBAHT, hivyo ninajua ni jinsi gani wanapambana kuwanusuru watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi, lakini baadhi ya watu hawajabadilika, wanaamini huo ni uchafu," anasema.

"Kitendo cha baadhi ya wazazi na walezi kuficha watoto wenye ulemavu huo na kinasabisha tatizo kuendelea kuwa kubwa, lakini kama wangepata elimu ya kutosha na kuizingatia, ingawa ni rahisi kulimaliza," anasema Theresia.

Anasema, mtoto anapozaliwa na ulemavu huo halafu akafichwa, hali hiyo inaweza kusababisha tatizo la kiafya kuwa kubwa na kumfanya asiweze kupelekwa shule kupata elimu.

"Mimi niko MOI, pia ninafanya kazi na ASBAHT, hivyo ninajua ni jinsi gani wanapambana kuwanusuru watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi, lakini baadhi ya watu hawajabadilika, wanaamini huo ni uchafu," anasema.

Ofisa Maendeleo huyo, anawaalika watu kufika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam kuanzia Oktoba 21 hadi 25, ili kupata elimu sahihi kuhusu chanzo cha ulemavu huo.

**HAKUNA USHIRIKINA**

Dk. Seif Lali kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, anasema ulemavu huo hauna uhusiano na ushirikina, kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakiamini, bali ni mambo ya kiyasansi.

"Ukosefu wa elimu sahihi ya kuzingatia lishe bora, hasa matumizi ya vyakula vyenye wingi wa vitamini ya foliki asidi vinavyopatikana katika maeneo mengi, ndiyo chanzo cha ulemavu huo," anasema Dk. Lali.

Anafafanua kuwa mwanamke anayetarajia kushika ujauzito, anatakiwa kula vyakula vyenye wingi wa foliki asidi kama mboga za majani kuanzia mchicha, spinachi, kabichi na nyingine nyingi.

"Kwa upande wa matunda, yapo maembe, maparachichi, mapapai na ndizi, lakini na nafaka kama mahindi, mihogo na mazao jamii ya kunde, pia mayai, samaki, nyama na maini. Ni muhimu kumeza kidonge cha foliki asidi kila mara kabla, wakati na baada ya ujauzito," anasema.

Anafafanua kuwa vyakula hivyo vianze kuliwa miezi miwili na nusu au mitatu kabla ya kubeba ujauzito na kuongeza kuwa ipo haja ya kuwawahisha watoto hospitalini pale mzazi anapoona dalili za ulemavu huo.



# Waombwa kusaidia uchangiaji wa damu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kujitokeza kuchangia damu kutokana na kuwapo kwa mahitaji makubwa katika vituo vya afya na hospitali nchini.

Msimamizi wa Kitengo cha Damu Salama Kanda ya Kati, Dk. Leah Kitundya, alitoa wito huo kwenye uchangiaji damu uliofanywa na Taasisi ya Kiislamu ya Jumuiyatul ya Akhlaaqul Islaam (JAI).

Alisema kwa mwezi Mkoa wa Dodoma unatakiwa kuwa benki ya damu kiasi cha chupa 1,000 hadi 1,500 lakini kiasi kinachokusanywa ni chupa 800 hadi 900 kwa mwezi.

Msimamizi huyo alisema kutokana na mahitaji yalipo nchini Watanzania wanatakiwa kuendelea kujitokeza katika matukio ya uchangiaji damu ili kuokoa maisha ya watu.

Alisema mahitaji ya damu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa mbalimbali pamoja na majeruhi wa ajali bado yako kwa kiwango kikubwa hali ambayo jamii inatakiwa kuendelea kujitolea bila kusita ili kuokoa maisha ya watu.

"Kawaida damu ina muda wake wa kuishi na inatakiwa kuishi siku 35, lakini haijawahi kutokea damu ikamwagwa kwakuwa inatumika na kuisha ndiyo maana tunasema kuwa lazima watu waendele kujitokeza katika uchangiaji," alisisitiza.

Naye Mratibu Mkuu JAI Taifa, Athumani Massanga, akizungumza kwenye tukio hilo la kuchangia damu, alisema kuwa jumuiya hiyo imeamua kumuenzi Baba wa Taifa kwa kujitolea damu ili kuokoa maisha ya watu wenye uhitaji.

Massanga, alisema kitendo cha kutoa damu ni sehemu ya ibada kwa kuwa tone moja la damu litaokoa uhai wa mtu au kumpotezea maisha ikiwa atakosa.

Hata hivyo, alisema pamoja na utoaji wa damu kwa kila wakati pia jumuiya hiyo ya JAI inafanya mambo mengi ya kusaidia jamii.

"JAI imekuwa ikijipambanua kama Jumuiya ya tabia njema za Kiislaam kwa misingi ya kuwasaidia watu wote wenye uhitaji bila kujali itikadi za kidini, rangi, ukabila, itikadi za kisiasa."

"Sisi tumekuwa tukitoa misaada kwa nyanja mbalimbali kwa jamii mbalimbali kwa kuamini kuwa kila binadamu anahitaji msaada wa mtu mwingine," alisema.

Aidha, alisema pamoja na kujitolea damu kama sehemu ya ibada jumuiya hiyo imekuwa ikihamasisha jamii kupata chanjo ya UVIKO -19 ili kujikinga na ugonjwa huo.

Kwa upande, Mratibu wa JAI Mkoa wa Dodoma, Fauz Baadhafan, alisema lengo la mkoa ni kupata chupa za damu 100 mpaka 150.

"Tumeandaa zoezi hili ikiwa ni kumbukumbu ya miaka 22 tangu kufariki Baba wa Taifa lengo ni kupata angalau chupa za damu salama 100 hadi 150 na kufanya hivyo kutakuwa ni sehemu ya ibada ya uokoaji maisha ya watu,"alisema.

# Watakiwa kushiriki udhibiti matumizi holela dawa kinga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa afya nchini wametakiwa kushiriki kikamilifu kwenye Mpango wa Taifa wa kudhibiti matumizi holela ya dawa kinga (antibiotics) kwa jamii.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mfamasia Bartazar Stanley alipokuwa akitoa mada ya kukuza uelewa wa ukinzani wa antimicrobial (AMR) katika jamii kwa Mkoa wa Dodoma kwenye Kongamano la Afya Tanzania (THS) ikiwa ni miongoni mwa mawasilisho ya Mradi wa HPSS-Tuimarishe Afya unaotekelezwa na Shirika la Swiss TPH kwa ufadhili wa Shirika la Ushirikiano na Maendeleo la Uswisi (SDC).

Alisema bado suala la usugu wa dawa hizo halijapewa umakini wa kutosha na umma hauna uelewa wa kutosha kuhusu hilo hali ambayo inachangia kuongezeka kwa matumizi hayo yenye athari kiafya.

Alibainisha kuwa moja ya malengo ya kimkakati ya mpango huo ni kudhibiti matumizi holela ya dawa kinga na kuimarisha ufahamu wa umma na uelewa wa AMR. "Mpango wa Kupambana na Utumiaji wa Antimicrobial (RBA Initiative) imekuwa kinara wa utumiaji wa vijana kama mawakala wa mabadiliko ili kuongeza uelewa wa AMR, kukuza mabadiliko mazuri ya tabia na hivyo kupunguza kutofaulu kwa matibabu," alisema.

Hata hivyo, alisema mradi wa kuwajengea uwezo kwa wanafunzi wa shule za sekondari mkoani Dodoma umekuwa na mafanikio.

"Sio rahisi kumbadili mtu kadri umri unavyoongezeka, ndivyo wanavyozidi kushikilia njia alizozoea, watoto wa shule wako katika miaka ya ukuaji, ambao ni wakati sahihi wa kutoa maarifa na njia bora ambayo yataongoza tabia zao maishani," alisema.

Alifafanua kuwa ikiwa vijana wanaohusishwa na kujengewa uwezo wataongeza maarifa na ufahamu wa jamii kuhusu AMR kama wakala wa mabadiliko.

Naye Mfamasia, Erick Venant alisema katika utafiti uliofanywa kwa wanafunzi wa shule za sekondari mkoani Dodoma uliokuwa kwenye maeneo matatu ya ufahamu wa njia za kupunguza AMR, uelewa kwamba antibiotics haiwezi kutumika kutibu mafua na sababu zinazochangia ukinzani wa dawa kinga.

Alisema kabla ya kupewa mafunzo, uelewa katika vipengele vyote ulikuwa chini ya asilimia 30 na baada ya miezi mitatu baada ya mafunzo uelewa uliongezeka hadi kuwa zaidi ya asilimia 90.

"Klabu za shule za AMR ni chombo bora cha kuongeza uelewa na kupunguza tatizo la usugu wa dawa, kutilia mkazo kutaongeza ufahamu na uelewa mpana katika jamii," alisema.




Ofisa Masoko na Mauzo wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Peter Mobe (katikati), akimwonyesha mafuta ya kula ya alizeti yanayozalishwa na viwanda vya bodi hiyo mkazi wa Dodoma, George Mhilu, alipotembelea banda hilo, katika maonyesho ya wazalishaji bidhaa za mazao ya kilimo yaliyofanyika jana, jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TAKUKURU yatahadharisha kuhusu rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imeeleza utekelezaji wa maboresho ya sheria ya makosa ya rushwa ulivyo kwa sasa, huku ikiwataka Watanzania kujiepusha na kujipatia mali kwa njia ya rushwa.

Akizungumza jana na klabu za wanafunzi za kupinga rushwa, Mkuu wa Takukuru mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, alisema katika maboresho ya sheria ya rushwa kwa sasa makosa 23 kati ya 24 ni ya uhujumu uchumi.

"Maana yake ni kwamba ukipelekwa mahakamani na kutiwa hatiani adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 20 na hakuna faini, hii adhabu sio ndogo, huko tunakokwenda, kwasasa tunaendelea na makosa ya kupeleka watu mahakamani ambao walitenda makosa hayo sheria ilikuwa bado haijapitishwa."

"Kwa mujibu wa sheria huwezi kumshtaki mtu kwa makosa aliyoyatenda kabla ya sheria kutungwa, hawa wataendelea kushtakiwa na kuhukumiwa kwa adhabu zilizowekwa huko nyuma sio sasa hivi," alisema.

Aidha, alisema mtu anayejipatia mali kwa njia ya rushwa anapotiwa hatiani taasisi hiyo hufanya uchunguzi wa mali zake zote na kuiomba Mahakama kutaifisha mali zake zote.

"Hamna kitu kinachouma kama kunyang'anywa mali zako, sehemu ambayo itawauma sana watu wanaohusika na vitendo vya rushwa ni utekelezaji wa sheria hiyo ambayo ipo,"alisema.

Aliitaka jamii kuwa makini na kujiepusha na vitendo hivyo ili wasiangukie mikononi mwa sheria hiyo. "Naomba jamii itambue kuwa kuna sheria mpya hivyo ni vema watu wakaitambua ili isiwagharimu," alisema Kibwengo.

Hata hivyo, alizitaka klabu hizo kupambana na rushwa ili kumuenzi Hayati Mwalimu Julius Nyerere ambaye alikuwa mzalendo na mpinga rushwa.

Alisema hapa jijini Dodoma kuna klabu nyingi za rushwa ambazo zinasaidia kupambana na rushwa ikiwamo kutoa elimu.



# Wanafunzi Ikumbi wasitisha masomo kwa kuwekewa uzio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI 40 wa Shule ya Msingi Ikumbi Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamesitisha masomo baada ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini (TAA) kuweka uzio kuzunguka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe na kuziba njia waliyokuwa wakiitumia kwenda na kurudi shuleni.

Wanafunzi hao ni wakazi wa kitongoji cha Iwejele katika kijiji cha Songwe ambao wamelazimika kusitisha kwenda shule kwa kuogopa kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 13 kutoka kwenye kitongoji hicho kwenda shuleni kwa kuzunguka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Wakizungumza na Nipashe, wakazi wa eneo hilo walisema kabla ya kuwekwa uzio katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, wanafunzi walikuwa wakisafirishwa na gari la TAA kwenda na kurudi shuleni ili kuwavusha salama uwanja wa ndege.

Willy Daniel mkazi wa kitongoji cha Iwejele, alisema baada ya TAA kukamilisha zoezi la uwekaji wa uzio kwenye uwanja huo, huduma ya kuwasafirisha wanafunzi hao kwenda na kurudi shuleni imesitishwa ghafla.

"Wakati ule hawajaweka uzio, walikuwa wakileta gari la uwanja wa ndege linawachukua watoto linawapeleka shuleni na kuwarudisha nyumbani baada ya masomo, lakini walipokamilisha ujenzi wa uzio wameacha kuleta gari na sasa watoto wanatakiwa kutembea kwa miguu kuzunguka uwanja wa ndege kwenda na kurudi," alisema Daniel. Kwa upande wake Juma Watson alisema njia ya kuzunguka uwanja wa ndege licha ya kwamba ni ndefu, pia ina makorongo makubwa, mito na vichaka vinavyoweza kuhatarisha usalama wa watoto hao.

"Baadhi ya watoto ni wadogo hawawezi kuhimili kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 13 kwenda shuleni na pia njia wanayotakiwa kupita ni hatarishi kwa vile ina makorongo makubwa, kuna mito na machaka mengi ambapo lolote linaweza kuwatokea watoto wetu," alisema Watson.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ikumbi, Ntasya Titus alisema kitongoji cha Iwejele pekee kina wanafunzi 36 na maeneo ya jirani na kitongoji hicho kuna wanafunzi wanane na kufanya idadi yao kuwa 44 ambao wote wana zaidi ya wiki mbili hawajahudhuria masomo.

Mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Ikumbi, Eliuda Noah ambaye ni miongoni mwa walioamua kusitisha masomo, alisema walijaribu kwenda shuleni kwa miguu na walitembea umbali mrefu waliporejea nyumbani walijikuta wamechoka na miguu imevimba.

"Tulitembea umbali mrefu kwenda shuleni, kwanza tulichelewa kufika na kukuta wenzetu wameshaanza masomo na wakati wa kurudi tulirejea nyumbani usiku tukiwa tumechoka, asubuhi tuliamka tukakuta miguu imevimba na bado tulitakiwa kutembea tena kwenda shule kwa kweli tunashindwa kwenda shuleni maana ni mbali sana," alisema Eliuda.

Baadhi ya kinamama wazazi wa watoto waliositisha masomo, wameiomba serikali kuingilia kati suala hilo ili watoto wao waweze kuendelea na masomo.

Mmoja wa wazazi hao, Juliana Mwanula aliiomba serikali kuwasaidia usafiri kwa ajili ya wanafunzi hao kwenda shuleni au kufanya uamuzi wa kuwajengea darasa kama shule shikizi kwenye kitongoji chao kwa ajili ya kunusuru masomo ya wanafunzi hao. Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, Danstan Komba, hakutaka kuzungumzia suala hilo kwa madai kuwa lipo chini ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua.

Chuachua alipotafutwa na gazeti hili alikiri kulitambua tatizo hilo na kudai kuwa serikali bado inaendelea kulifanyia kazi ili kuhakikisha wanafunzi hao wanaendelea na masomo.

Kitongoji cha Iwejele kilijikuta kikijitenga na Kijiji mama cha Songwe baada ya eneo lililo katikakati kutwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege huku baadhi ya huduma muhimu za kijamii kama shule vikibakia kwenye kijiji mama cha Songwe.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akinunua dagaa katika Soko la Igawilo jijini Mbeya hivi karibuni wakati wa ziara ya kamati ya utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa chai, kahawa, mboga na matunda ujulikanao kwa jina la AGRI-CONNECT. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mil. 286/- kujenga mradi wa maji Ikukwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetenga Sh. milioni 286 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika Kata ya Ikukwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya utakaohudumia vijiji viwili vya Ikukwa na Itende Juu.

Meneja wa Wakala wa Maji mijini na vijijini (RUWASA) wa halmashauri hiyo, Mhandisi Sambwe Sijabaje, alisema hayo wakati wa ziara ya Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Rashid Chuachua pamoja na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza.

Alisema mradi huo utakuwa suluhisho la tatizo la maji katika kata hiyo na wataanza kuutekeleza hivi karibuni ili kuwaondolea wananchi wa kata hiyo kero ya huduma hiyo.

"Fedha zimeshatengwa kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha na wananchi wa kata hii wataondokana na tatizo la upatikanaji wa maji, nawaomba sasa hivi waendelee kuvumilia," alisema Sijabaje.

Alisema vitajengwa jumla ya vituo 17 kwenye vijiji vyote viwili ambavyo wananchi watakuwa wanavitumia kuchota maji na kwa wananchi wenye uwezo wataingiziwa mpaka majumbani mwao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Chuachua aliagiza mradi huo ukikamilika taasisi zote za umma lazima ziingiziwe huduma hiyo ya maji ikiwamo shule na kituo cha afya cha kata hiyo ambacho kimejengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.2.

Aliagiza mradi huo uanze kutekelezwa haraka ili kuwaondolea wananchi hao shida ya kufuata maji mbali na makazi yao na kutekeleza sera ya serikali ya kuwatua ndoo ya maji wanawake.

"Kituo chetu cha afya kinahitaji maji hivyo hakikisheni mnaunganisha pia hapo pamoja na shule zote, sasa nawaomba wananchi nanyi mwendelee kujitolea nguvu zenu ikiwamo kuchimba mitaro na kubeba mchanga," alisema Dk. Chuachua.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Njeza alisema tatizo la maji ni miongoni mwa matatizo yanayomnyima usingizi kwenye jimbo hilo kutokana na wananchi kuhangaika na katika mikutano yake mingi wananchi wanakidai huduma hiyo.

# UWT yahamasisha utalii wa ndani kutembelea hifadhi

**Na Nebart Msokwa,** IRINGA

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya, umeanza kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutembelea hifadhi mbalimbali za taifa pamoja na maeneo yenye vivutio vya kihistoria ili kukuza sekta hiyo na kuongeza pato la taifa.

Mwishoni mwa wiki wajumbe zaidi ya 30 wa umoja huo kutoka katika wilaya zote za mkoa huo walitembelea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha mkoani Iringa na kujionea vivutio mbalimbali vilivyomo katika hifadhi hiyo wakiwamo wanyama, ndege na mimea.

Wanawake hao walisafiri kwa kutumia Shule ya Paradise Pre and Primary School katika Mamlaka ya Maji mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya ambayo ni miongoni mwa wadau waliodhamini ziara hiyo.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya, Oliva Kibona, alisema ziara hizo za kutembelea Hifadhi za Taifa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya UWT ambayo itahitimishwa hivi karibuni mkoani Pwani.

Alisema baada ya kutembelea Hifadhi ya Ruaha wanakusudia kufanya ziara zingine kwenye vivutio vingine vikiwamo vilivyopo visiwani Zanzibar na lengo la umoja huo ni kuhamasisha utalii wa ndani.

Alisema hifadhi za taifa zimekuwa zikitembelewa na watalii kutoka nje ya nchi na kutegemea watalii wa kigeni imeonekana kuwa ni tatizo hasa kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa corona.

"Tulipanga kuja wajumbe zaidi ya 100, lakini kumetokea matatizo ikiwamo misiba na hivyo baadhi ya wajumbe wameenda huko hawa ni wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UWT mkoa na madiwani wa kata mbalimbali za mkoa wetu," alisema Kibona.

Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UWT Mkoa wa Mbeya, Taimu Mwaibako, alisema katika ziara hiyo waliona vivutio mbalimbali vya utalii wakiwamo wanyama ambao walikuwa hawajawahi kuwaona kabla.

Alisema waliwaona tembo wakubwa wa hifadhi hiyo, twiga, viboko, mamba na ndege mbalimbali wenye rangi na sauti za kuvutia na akawataka Watanzania waendelee kutembelea vivutio hivyo ili kuliingizia taifa fedha.

Taimu alisema pamoja na kuwaona wanyama hao pia walijifunza tabia mbalimbali za wanyama walioko kwenye hifadhi hiyo ambazo walielezwa na waongoza watalii.

"Tumefurahi maana tumejifunza mambo mengi sana kwenye hii hifadhi, tunawashukuru waliotuwezesha kufika huku tunaomba waendelee kutusaidia kuona vivutio vingine na tunawashauri na wananchi wengine watembelee vivutio hivi," alisema Taimu.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Kandete katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, Butulye Kagenda, aliiomba serikali kuboresha barabara ya kutoka Iringa Mjini mpaka katika hifadhi hiyo ili kurahisisha usafiri.

Alisema baadhi ya maeneo ya barabara hiyo yameharibika kiasi kwamba baadhi ya magari hayawezi kupita kwa urahisi na hali hiyo inaweza ikakatisha tamaa baadhi ya watalii.





# Watakiwa ubunifu kuwavutia watalii

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullla, amewataka wadau wa sekta ya utalii kubuni mbinu mpya zitakazosaidia kuwavutia watalii kurudi tena kuitembelea Zanzibar.

Hemed aliyasema hayo Jana wakati akilifungua kongamano la wadau wa utalii Zanzibar lililofanyika katika Hotel ya Golden Zanzibar.

Aliwashauri wadau hao kubuni mbinu mpya zenye kuzingatia ushindani kwa kuibua vivutio vipya sambamba na kuviimarisha vivutio vyengine ili viwe na mazingira yatakayowashawishi watalii kurudi tena kuitembelea Zanzibar.

Makamu wa Pili huyo aliwaomba wadau wa utalii kutoridhika na dhana kuwa Zanzibar inajitangaza yenyewe bali inapaswa kuchukua hatua za makusudi ili kuingia katika ushindani kutokana na nchi zingine kuendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutangaza nchi zao.

Aidha, aliupongeza uongozi wa Jumuiya ya kitaifa ya wafanyabiashara Zanzibar kwa kushirikiana na UNDP kwa hatua wanazozichukua katika kurudisha ustawi wa sekta ya utalii Zanzibar kwa ajili kuinua uchumi.

Alisema sekta ya utalii Zanzibar iliathiriwa na UVIKO-19 ambapo ilikuwa ikitegemea kwa asilimia kubwa ya ukuaji wa uchumi wake kupitia sekta hiyo.

Alieleza kuanguka kwa soko la utalii Zanzibar kulipelekea kusimama kwa ajira nyingi za wananchi kuliko sababishwa na kufungwa kwa hoteli, jambo lililopelekea kushuka kwa pato la serikali kwa ajili ya kutoa huduma za msingi kwa wananchi wake.

Alikemea vikali tabia inayofanywa na baadhi ya watembeza watalii kwa kuharibu viumbe hai vya baharini hali inayopelekea kuharibu rasilimali za bahari.

Naye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, alisema wizara imekuwa na utamaduni wa kushirikiana na wadau tofauti katika kufufua utalii ulioathiriwa na ugonjwa wa UVIKO-19.

Alieleza kuwa, kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 kuikumba dunia imesababisha Jumuiya za kikanda ikiwemo Afrika Mashariki na SADC kuwa na vikao vya pamoja katika kujadili na kutathmini namna bora ya kufufua utalii katika nchi zake.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya kitaifa ya wafanyabiashara Zanzibar, Ali Amour, alisema kuwa katika mwaka 2020 sekta ya utalii ilitarajiwa kuchangia Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia 35 pia ilitarajiwa kukusanya asilimia 80 ya mapato pamoja na kuajiri watu wapatao 100,000, lakini kutokana na janga la UVIKO-19 lilisababisha kushindwa kufikiwa kwa malengo hayo.

Mwakilishi kutoka UNDP, Rukia Wadoud, alisema UNDP inaipongeza serikali ya Zanzibar kwa ushirikiano wake inautoa kwa kushirikisha wadau kutoka taasisi binafasi na kuahidi kuwa UNDP itaendelea kutoa ushirikiano wake kwa serikali ili kuinua maendeleo ya sekta ya utalii Zanzibar.

## Serikali yaanika mafanikio TASAF

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umepata mafanikio makubwa baada ya kujikita katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili wananchi.

Baadhi ni kinamama na watoto katika sekta ya afya. Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Thabit Idarous Faina, wakati akikagua mradi unaotekelezwa na TASAF wa ujenzi wa Hospitali ya Kiendwa Pemba ambayo inajengwa kwa kutumia fedha za TASAF.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga kuzitumia vizuri fedha za TASAF awamu ya pili unaotarajiwa kutekelezwa hivi karibuni ambao fedha zake zimejikita katika kusaidia miradi inayowahusu jamii moja kwa moja.

Aliwataka watendaji watakaokabidhiwa jukumu la kutekeleza mpango wa awamu ya pili ya mfuko wa TASAF kuwa makini sana na kuona fedha zilizotengwa zinatumika katika malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

Alisema miradi ya ujenzi wa hospitali ikiwamo za kinamama na watoto ni mkombozi ambazo zimekuwa zikisaidia na kuwapatia huduma makundi mbalimbali ikiwamo wanawake na watoto.

"Nimefurahishwa na maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Kiendwa ambayo inajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambazo zitasaidia kutoa huduma kwa kinamama na watoto," alisema.

Naye Mkuu wa TASAF Pemba, Mussa Said, alisema mradi huo hadi sasa umetumia jumla ya Sh. milioni 85 na utakapomalizika Desembaa unatarajiwa kutumia Sh. milioni 347.

Said alisema hadi kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo itakuwa na huduma mbalimbali ikiwamo uchunguzi wa magonjwa mbalimbali na upimaji wa damu na huduma kamili za kinamama na watoto.

Aidha, alisema katika mradi huo nyumba ya daktari itajengwa kwa ajili ya kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa muda wote.

"Mradi huu ni mkubwa ambao utahusisha huduma nyingi zinazopatikana katika hospitali hiyo yenye sifa ya wilaya kwani kinamama pamoja na watoto watapata matibabu yote kamili," alisema.




Mke wa Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Saib (kushoto), akikagua maonyesho ya wanafunzi wa chekechea Shule ya Kidutani Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Watumishi waonywa usimamizi wa mitihani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema haitamvumilia mtendaji yeyote atakaye kwenda kinyume na mwongozo, kanuni na taratibu za kazi za usimamizi wa mitihani ya Taifa ya darasa la nne, sita na kidato cha pili inayotarajiwa kuanza Oktoba 25 ya mwaka huu.

Akifungua semina elekezi ya wasimamizi wa mitihani katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Lumumba, Waziri wa Wizara hiyo, Simai Muhammed Said, alisema lengo la mitihani hiyo ni kuhakikisha wanafunzi wanatumia vizuri akili zao, ili serikali kupata wataalamu bora na weledi wa baadaye.

Alisema si vyema kwa walimu hao kutumia nafasi zao kwa kuharibu kazi hiyo, hivyo atakayebainika kwenda kinyume na maelekezo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kifungo na faini isiyopungua shilingi milioni moja au vyote kwa pamoja.

Alisema kuwa lengo kuu ni kuona mafanikio ya mwaka mzima katika ufundishaji wa watoto na kuona kwa kiasi gani wamefanikiwa katika kuwasaidia watoto hao na kujua pia nao wamepokea vipi kile walichofundishwa.

Simai alisema kutokana na kuwa na juhudi, weledi, uaminifu na uadilifu walionao katika utendaji wa kazi zao, wameonekana kuwa wanaafiki na ndio maana wamebahatika kuteuliwa kusimamia kazi hiyo maalumu ya kitaifa.

Hivyo alisema matarajio ya wizara kuwa watonesha kwa vitendo imani waliyopewa kwa kufanya kazi hiyo kwa uaminifu na uadilifu pamoja na kufuata sheria, kanuni na miongozo ya mitihani watakayopewa chini ya usimamizi wa Baraza la Mitihani la Zaznibar.

Naye Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani Zanzibar, Zubeir Juma Khamis, aliwataka walimu hao kuwa makini na kutojihusisha na vitendo vya udanganyifu ambavyo vinaweza kuitia hasara serikali.

Aidha, alisema kuwa si vyema kujaribu kumsaidia mwanafunzi, shuleni kwa sababu za kufanya vizuri na kuwataka kuwaacha watumie ujuzi, maarifa na stadi walizo nazo katika kufanya mitihani yao hiyo.

"Taifa hili linahitaji wataalamu katika fani mbalimbali kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ambapo chimbuko lake ni kupata wanafunzi wenye elimu bora," alisema Zubeir.

Kwa upande wake Mwanasheria wa Baraza la Mitihani Zanzibar, Ummukulthum Omar Ali, aliwataka wasimamizi hao kuhakikisha kuwa kiapo walichoapa mbele ya waziri, kinaanza kufanya kazi tokea muda walioapa mpaka kutoka kwa matokeo, hivyo aliwataka kufuata sheria zote walizoelekezwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

TAJIRIKA FUGA MAJOGOO WA KIENYEJI WEUPE WA NYAMA WAITWAO BOVANS TOKA PARANGU FARM WANAOHIMILI MARADHI NA WANAOVUNWA HARAKA UPIGE PESA. VIFARANGA WAPO WA SIKU HADI MWEZI MMOJA KWA ODA.

**TUPIGIE: 0673 722 823**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**RUKAIYA MALICK RUSHAGAMA** anatangaza kupotea kwa Result Slip yenye index namba **S.526/0653** iliyotolewa na **MRINGA SEKONDARI** mwaka 2021. **Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/MBU/RB/498029/2021.**

116518902

## KUPOTEA KWA VYETI



**JUSTINE JONAS KIMBUNGA** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S.0896/0049** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya KIZUKA(TPDF) HIGH mwaka 2012 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0142/0622** kiichotolewa na baraza la mtihani kupitia shule ya GALANOS HIGH mwaka 2015,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **KW/RB/4987/2021**

116518702

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**HERRY FADHILI KALISA** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha nne yenye index namba **S0341/0116** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **SANGU mwaka 2020,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/MAG/RB/499916/2021**

116520002

## KUPOTEA KWA CHETI



**SWEETGLAD SADICK TARIMO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1619/0083 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **VICTORY mwaka 2015,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/MAG/498925/2021**

116520102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KANANJI CHINGWALU SAID** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 957 CKM** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Control No: **9910830572405.**

116519602

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JULIUS MICHAEL LUNGU** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 631 CDK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **SO/RB/2021.**

116519302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MAGODO NAMBA 177 YA 2021**
**(yatokanayo na maombi no 69/2019)**

**MARIAM A. KAMBI**
**(Msimamizi wa mirathi ya marehemu**
**ASHA OMARI BUHUMU)…….........MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JUMANNE RAMADHANI CHANG`ANDU**
**(msimamizi wa mirathi ya marehemu**
**RAMADHANI OMARY CHANG`ANDU)**
**BARAKA YOHANA PEARSON ……………MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**BARAKA YOHANA PEARSON** Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 08/11/2021 mbele ya mwenyekiti E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 10 mwezi October 2021

E.MOGASA
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

116519302

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**

**(CAP.117)**

**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED.I HAPPYNESS ELIZABETH SYLVESTER of P.O. BOX 116 CHATO.DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly renounce relinquish and abandon the use of my former name of **HAPPYNESS SYLVESTER AROKO** which are used in National Identification Authority **(NIDA)** with **Re. No.19930521-14112-00001-11** and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of **HAPPYNESS ELIZABETH SYLVESTER** The name of **HAPPYNESS ELIZABETH SYLVESTER** is used in my certificate of Secondary Education with Index **No.s.1877-0020**
**IN WITNESS WHERE** of I herein substitute my old name **HAPPYNESS SYLVESTER AROKO** by the new name of **HAPPYNESS ELIZABETH SYLVESTER** and have set my hand at **Geita this 06 day of, October 2021**
**SIGNED and DELIVERED** by the said **HAPPYNESS ELIZABETH SYLVESTER** Who is known to me personally/identified to me by…… the latter being known to me personally in my presence this 06 day of October 2021.............................. **DEPONENT**

Name: Rehema E. Malecha
Signature: ..........
Postal address: ......72 Geita
Qualification: COMMIONER FOR OATH

116519202

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

Mariam Hamis mkazi wa Ngokolo Manispaa ya Shinyanga.

Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba 608 Kitalu "V" Kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga chenye jina la Elias Masaka.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi Kilichopo Karibu au awasiliane na Mariam Hamis kwa simu namba 0623881161

**Rbnamba Shy/RB/2021/**
**Control namba 991174814609**

116519402

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 20 OF 2021**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**AGNESS ANTONY ISMAIL**

By 1. FARIDA HARUNI CHANDE
2. ……………………………………

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration ) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 21 day of 10 ……………2021
Dated at Morogoro this 30 day of 9………….2021

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO……. 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**ARISTIDE ANTONY MUNISHI**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATOR OF A SMALL ESTATE BY**
**BONIFACE ANTONY MUNISHI**
**FORM 58**
**APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATOR OF SMALL ESTATE**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 day of 11,2021.

**Dated at Dodoma this 18 day of October 2021**

116519702

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 116 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BADRUDIN HASHAM LAKHANI**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**BILQUIS LADAK**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji /mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 11 mwezi wa 11 mwaka 2021
Imewasilishwa dar es salaam leo tarehe 11 mwezi 10 mwaka 2021

NAIBU MSAJILI

116519102




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kijiji Lukenge chaahidiwa kumalizwa kero ya maji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MENEJA wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Pwani, Beatrice Kasimbasi, amekiri kuwapo kwa tatizo la maji katika Kijiji cha Lukenge wilayani Kibaha na kwamba mradi unatekelezwa na hivi karibuni shida hiyo itaisha.

Kasimbasi alieleza hayo jana alipokuwa akiongea na waandishi waliofika ofisini kufuatilia hatima ya wananchi wanaokesha kwenye bwawa huko Lukenge wakisaka maji.

Meneja huyo alisema mradi wa maji Mlandizi Mboga unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), unaotarajiwa kukamilika hivi karibuni utahudumia vijiji zaidi ya 90 kikiwamo cha Lukenge.

Katika hatua nyingine meneja huyo alisema katika fedha za Uviko-19 zaidi ya Sh. bilioni 4.24 zimetengwa kwa Mkoa wa Pwani kwa ajili ya miradi ya maji kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Kasimbasi alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 mkoa huo awali ulitengewa Sh. bilioni 17 kwa ajili ya kutekeleza miradi 29 na baada ya ongezeko la fedha za Uviko-19, miradi 54 inatarajiwa kutekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 21.92.

"Utekelezaji wa miradi hii utaongeza asilimia za usambazaji wa maji kufikia 86 baada ya kukamilika miradi 54," alisema.

Alisema RUWASA wana mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uchangiaji wa huduma za maji ili miradi inayotekelezwa iwe endelevu.

Kasimbasi alisema itatolewa pia elimu ya matumizi ya majisafi na salama ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Mwanzoni mwa mwezi huu Nipashe ilifika katika Kijiji cha Lukenge na kushuhudia wananchi wakisubiri maji kwa zaidi ya saa 12 kutokana na kero ya maji iliyopo katika kijiji hicho.

**Kasimbasi alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 mkoa huo awali ulitengewa Sh. bilioni 17 kwa ajili ya kutekeleza miradi 29 na baada ya ongezeko la fedha za Uviko-19, miradi 54 inatarajiwa kutekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 21.92.**



Moja ya gari likipita pembeni ya mti wa ajabu wa asili ambao ulikuwa ukitumiwa kufanya matambiko na jamii kwa ajili ya utatuzi wa masuala mbalimbali uliopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, mti huo kama unavyoonekana upo katikati ya barabara baada kushindikana kung'olewa kwa mashine na zana mbalimbali kutokana na kile kinachoelezwa una mazingara. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Shahidi: Sabaya alijiita ofisa TISS mkusanya kodi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KARANI katika gereji ya mfanyabiashara Francis Mroso, Philemon Kazibira (64), ameieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, kwamba aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, alifika katika ofisi yao akidai kuwa ni Ofisa wa Usalama wa Taifa (TISS), anayeshughulika na ukusanyaji wa kodi.

Karani huyo ambaye ni shahidi wa nne wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Ole Sabaya na wenzake sita, alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Patricia Kisinda.

Washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29), Nathan Msuya (31) na wanakabiliwa na mashtaka matano.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Othmed Mtenga, shahidi huyo alidai kwamba ni mkazi wa Kata ya Olorieni jijini Arusha na amefanya kazi ya ukarani katika ofisi ya Mrosso Injector Pump Services iliyopo Mbauda jijini humo tangu mwaka 2015.

Alidai Januari 20, mwaka huu, alipokea pampu aina Toyota 3L kutoka kwa kijana mmoja anayeitwa Watson Mwahomange na baada ya kuangalia pampu hiyo alimpa bei ya kutengeneza ni Sh.100,000 baada ya kuikagua.

"Baada ya kumpa bei halisi aliniambia kwamba anataka kuwasiliana na aliyemtuma na muda kidogo alirejea kwangu na kunieleza kwamba amekubaliana na bei na alilipa kiasi hicho cha fedha cha Sh. 100,000 na siku hiyo nilishindwa kumpatia risiti kwa kuwa mashine ya kielektroniki ilikuwa haifanyi kazi kutokana na shida ya kimtandao," alidai.

Shahidi huyo alidai kwamba Januari 22, katika ofisi yake walikwenda vijana wawili wakidai kwamba ni maofisa wa usalama wa taifa na wanahusika kukusanya kodi. "Walipojitambulisha kuwa ni maofisa wa usalama wa taifa niliwakaribisha na baada ya muda kidogo wakaniuliza kama mimi ndiye mwenye ofisi na kama tunalipaga kodi, pia walimuulizia mwenye ofisi na niliwajibu kwamba ametoka kidogo na walitaka kufahamu jina lake na niliwaeleza anaitwa Francis Mroso," alidai shahidi.

Kadhalika alidai kwamba baada ya muda kidogo kupita aliingia mtu wa tatu na mmoja wa wale vijana wawili walimpisha na aliketi kwenye kiti.

"Alipoingia mtu huyo nilimtambua kuwa ni Lengai Ole Sabaya kwa kuwa nilimwona kwenye televisheni akitekeleza majukumu yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai," alidai.

Shahidi huyo alidai kwamba Sabaya alimwagiza kumpigia simu Francis Mroso kuwa kuna wageni wapo ofisini kwake wanataka kuonana naye.

"Wakati tunamsubiri Mroso, Sabaya alimwagiza Watson, kumpelekea simu na alinionyesha picha yangu ambayo walinipiga wakati nikiwa natengeneza pampu muda huo nilikuwa nimekaa kwenye kiti pasipo kufahamu," alidai shahidi huyo.

Alidai kuwa Sabaya alimweleza kwamba wanafanya biashara bila ya kutoa risiti na Mroso alipoingia walianza kuzungumza jambo la kutokutoa risiti. "Sabaya alisema kwamba kwa kuwa wameshampata mwenye ofisi aliniambia mimi niondoke na kuagiza niache hapo kila kitu nilichokuwa nimebeba ikiwamo simu yangu ya mkononi na baada ya kuondoka sikufahamu nini kiliendelea na walizungumza hadi majira ya saa 8:00 mchana," alidai shahidi huyo.

Pia shahidi huyo alidai Sabaya alipomaliza mazungumzo aliondoka na ilipofika majira ya saa 10 jioni, Francis Mroso, alimpigia simu kumjulisha kwamba kuna kijana anaitwa Juma atakwenda ofisini hapo na ampatie kadi ya benki ya CRDB iliyopo kwa Murombo, jijini Arusha.

"Kijana yule alifika ofisini na nilimkabidhi kadi na alimpelekea mhusika sehemu ambayo alikuwapo na ilipofika saa 11 jioni, Mroso, alirejea ofisini akiwa katika hali ya uchovu kwa kuwa hakuwa na furaha siku hiyo, alionekana kuwa ni mtu mwenye huzuni," alidai shahidi huyo.

Katika hatua nyingine, shahidi huyo aliwatambua washtakiwa hao kwa kuwashika bega mahakamani, Sabaya (mshtakiwa kwanza) na Watson Mwahomange (mshtakiwa wa tatu) katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi.

Akihojiwa na Wakili wa Upande wa Utetezi, Mosses Mahuna, shahidi huyo alidai kwamba alimfahamu Watson kwa majina yake kwa kuwa alijitambulisha.

Alidai kwamba mshtakiwa wa tatu alikaa hapo gereji kwa saa tatu na wakati akimpatia pampu hiyo hakumsainisha kwa kuwa siyo utaratibu wao.

Pia alidai mtandao wa mashine ya kielektroniki ya EFD ulirejea Januari 22 mwaka huu, baada ya kupeleka kurekebishwa kwa wakala wa mashine hizo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Shahidi mwingine dereva bodaboda, mkazi wa Majengo jijini Arusha, Juma Nuhu (28), amedai kwamba alimwona Ole Sabaya, katika gereji ya Mroso, akiwa amening'iniza pingu katika suruali yake.

Kadhalika shahidi huyo, aldai aliona magari matatu likiwamo moja la serikali yakiwa yamepaki nje ya lango la kuingilia katika gereji hiyo.

Mwendesha bodaboda huyo, ambaye ni shahidi wa tano wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, alitoa madai hayo mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai anajishughulisha na kazi ya kuendesha bodaboda katika eneo la kona ya Majengo, jijini Arusha.

Alidai Januari 22, mwaka huu, akiwa katika eneo lake la kazi majira kati ya saa 4:00 asubuhi hadi saa 6:00 alipigiwa simu na Mroso kumtaka afike ofisini kwake akamchukue ili aende kukagua kazi sehemu.

"Nilifika na kumchukua kwenda kukagua kazi hiyo na mchana tulirejea ofisini kwake, majira ya saa 8:45 mchana na wakati tunaingia katika eneo hilo niliona gari kama la serikali aina ya STL limepaki nje ya lango la kuingili gereji ya Francis Mroso," alidai. Hata hivyo, alidai kwamba baada ya kumshusha Mroso, akiwa anasubiri kupewa maelezo alimuona Sabaya akitoka katika ofisi akiwa ameambatana na mfanyabiashara.

HABARI MICHEZO

# IBENGE ACHAMBUA UBORA WA SIMBA, AMTAJA MANULA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikianza kwa kutoruhusu bao (clean sheet) kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa RS Berkane, Mkongomani Florent Ibenge, amechambua ubora wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao akieleza ubora wao unapoanzia.

Simba ambayo msimu huu imeanzia raundi ya kwanza ya michuano hiyo, juzi iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Kwa matokeo hayo Simba sasa inahitaji ushindi, sare yoyote ama kutokubali kufungwa zaidi ya bao moja kwenye mechi ya marudiano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili wiki hii ili kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Akizungumza na mwandishi wetu aliyetaka kupata maoni yake baada ya Simba kuibuka na ushindi huo juzi, Ibenge ambaye msimu uliopita alikubali kipigo nyumbani na ugenini dhidi ya Simba kwenye hatua ya makundi akiwa kocha wa AS Vita ya kwao DR Congo, alianza kwa kueleza ubora wa mabingwa hao wa Tanzania uliopo.

Alisema Simba imekuwa ndiyo klabu yenye safu bora zaidi ya ulinzi na ubora wao unaanzia kwa kipa Aishi Manula, ambaye kiwango chake kimekuwa juu katika michuano hiyo.

"Nafikiri tangu msimu uliopita Simba ndiyo klabu yenye safu bora ya ulinzi kwenye mashindano haya ya CAF, ubora unaanzia kwa golikipa wao Manula," alisema Ibenge ambaye ameibomoa Simba kwa kumsajili kiungo wao mpishi wa mabao, Mzambia Clatous Chama.

Kauli hiyo ya Ibenge inathibitishwa na takwimu bora kabisa alizonazo Manula kwenye michuano hiyo, kwani katika mechi 12 ambazo ameidakia Simba kwenye michuano hiyo kuanzia msimu uliopita hadi sasa, hajaruhusu bao kwenye michezo nane ('clean sheets' 8).

Mechi ambazo hakuruhusu bao ni wakati Simba ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Plateau United ya Nigeria, kisha mchezo wa marudiano Uwanja wa Mkapa timu hizo zikitoka sare tasa.

Pia, wakati Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe na ushindi wa bao 0-1 ugenini DR Congo dhidi ya AS Vita kabla ya kurejea Dar es Salaam na kuifyatua Al Ahly ya Misri 1-0.

Mchezo mwingine ni katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Al-Merreikh kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na 3-0 dhidi ya Kaizer Chiefs, kabla ya juzi kusimama tena langoni wakati wakianza msimu mpya wa Ligi ya Mabingwa kwa kuicharaza Jwaneng Galaxy mabao 2-0 nchini Botswana.

SASA BRAZIL...



Miss Deaf Tanzania 2021, Hadija Kanyama, mzaliwa wa Muheza mkoani Tanga, akipokewa na Mkuu wa wilaya hiyo, Halima Bulembo (kushoto) pamoja na mamia ya wakazi wa Muheza katika Shule ya Msingi Mbaramo jana, baada ya kurejea akitokea Dar es Salaam, kushiriki mashindano ya Miss Deaf Afrika yalifanyika mwanzoni mwa mwezi huu, ambapo alishika nafasi ya pili iliyompa tiketi ya kwenda kushiriki mashindano ya dunia yatakayofanyika nchini Brazil Aprili mwakani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Penalti majanga matupu Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

PENALTI zote nne zilizopatikana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, zimeota mbawa na kuweka rekodi ya aina yake msimu huu.

Hadi kufikia leo hakuna penalti yoyote iliyojaa nyavuni, licha ya kwamba penalti nne zimetolewa na waamuzi kwenye mechi tatu.

Mechi kati ya Geita Gold dhidi ya Mtibwa Sugar iliyochezwa Jumamosi iliyopita, imeweka rekodi ya kuzaa penalti mbili mpaka sasa, lakini zote hazikutinga nyavuni, huku makipa wakigeuka kuwa mashujaa kwa kuzipangua.

Mkosi wa penalti kwenye Ligi Kuu msimu huu ulianza kwa nahodha wa Simba, John Bocco, aliposhindwa kuikwamisha kambani kwenye moja ya mechi za raundi ya kwanza dhidi ya Biashara United, Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, Septemba 28, mwaka huu, ambayo iliokolewa na kipa James Ssetuba, timu hizo zikitoka suluhu.

Straika wa Mbeya City, Eliud Ambukile, naye alikosa penalti Oktoba 3 kwenye mechi dhidi ya Mbeya Kwanza, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2. Ni penalti ambayo nayo ilipanguliwa na kipa Hamad Juma.

Jumamosi iliyopita kwenye mechi ya Geita Gold dhidi ya Mtibwa Sugar iliyochezwa Uwanja wa Shule ya Sekondari, Nyamkumbu mkoani Geita na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 wachezaji Boban Zirintusa na Raymond Masota walikosa penalti zao.

Boban aliikosesha Mtibwa Sugar tuta lililopanguliwa na kipa Khomein Aboubakar, huku Raymond Masota wa Geita Gold akipiga penalti iliyookolewa na kipa Abutwalib Mshelly.

## Wanawake watakiwa kujitokeza kujifunza gofu

**Na Tumaini Mafie, ARUSHA**

CHAMA cha Gofu nchini (TGU), kimewataka wanawake kujitokeza kushiriki mchezo huo huku kikitoa ombi lao kwa wadau wa michezo nchini kutoa hamasa ya zawadi ili kuwavutia kushiriki kwa wingi.

Akizungumza katika hafla fupi ya kuwapongeza washindi wa mashindano ya gofu yaliyofanyika jijini Arusha mwishoni mwa wiki, Katibu wa TGU, Mhandisi Magile Enock, alisema ushiriki wa wanawake katika mchezo huo ni mdogo ukilinganishwa na wanaume.

"Ni rai yetu kwa wadau wa michezo kuandaa zawadi zitakazowapa motisha wanawake ili kujiunga na mchezo wa gofu, lengo likiwa ni kuwa na usawa katika michezo nchini," alisema Enock.

Alisema TGU kwa sasa kimeruhusu mashindano ya gofu kuendelea kote nchini baada ya kuzuiliwa kwa miaka miwili kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa Covid-19 huku akisema baada ya michuano ya Arusha itafuatiwa na Lugalo Open inayotarajiwa kufanyika Oktoba 30 na 31, mwaka huu na kufuatiwa na TPC Open.

Naye mshindi wa jumla katika mashindano hayo, Victor Joseph kutoka Dar es Salaam, alisema pamoja na uwanja wa Gymkhana kuwa mgumu, anashukuru kuibuka mshindi na kujinyakulia kombe pamoja na zawadi mbalimbali.

## Azam yazitaka tatu za Namungo FC leo

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanatafuta ushindi wao wa kwanza baada ya kupoteza pointi nne katika michezo miwili, wakitoka sare dhidi ya Coastal Union na kukubali kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier, alisema wanahitaji kupata pointi katika mechi hiyo ili kuwa katika mwelekeo wa kufikia malengo yao.

"Sasa tunahitaji kushinda mechi yetu hiyo ya tatu, tufikie malengo yetu, kikosi kipo vizuri wachezaji wako fiti mbali na Price Dube ambaye ni majeruhi. Tunawaheshimu Namungo FC na tumefanyia kazi mapungufu yetu na ninaimani tutafanya vizuri," alisema Vivier.

Kwa upande wa nahodha msaidizi wa timu hiyo, Bruce Kangwa, alisema wamejiandaa vizuri na wanaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam leo.

"Tumefanya maandalizi ya kutosha na wachezaji tuko tayari kwa ajili ya mchezo wetu huo ili kupata matokeo mazuri na ushindi wetu wa kwanza kwa msimu huu," alisema Kangwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SOLSKJAER HATAFUKUZWA
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer hatatimuliwa licha ya raia huyo wa Norway kushinda mechi nne tu kati ya nane za Ligi Kuu England msimu huu. **(The Athletic)**

### BARCA YAMKATAA POGBA
BARCELONA haitamshawishi, Paul Pogba wa Manchester United wakati mkataba wa kiungo huyo Mfaransa utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu, kwa kuwa klabu hiyo ya Hispania haitaweza kumudu mshahara wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. **(AS)**

### BARKLEY ATAKIWA BURNLEY
KIUNGO wa zamani wa Chelsea na England, Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa kusajiliwa na klabu ya Burnley katika dirisha la Januari. **(Sun)**

### BALE ATAJWA ARSENAL
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 32, atapokea ofa ya usajili kutoka Arsenal katika dirisha la Januari. **(Defensa Central)**

### LEWANDOWSKI AWANIWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain itatupa karata kwa mshambuliaji wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, au mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye miaka 21, kama mbadala wa Mfaransa Kylian Mbappe. **(Le 10 Sport)**

### DE LIGT APELEKWA EPL
WAKALA wa mlinzi wa Juventus na Uholanzi, Matthijs de Ligt, Mino Raiola amezungumza na Klabu za Manchester City na Chelsea kwa matumaini ya kuchagiza uhamisho wa mlinzi huyo wa kati mwenye umri wa miaka 22. **(Calciomercato)**

### FATI MKATABA BARCA BADO
MAZUNGUMZO ya mkataba mpya wa mshambuliaji wa Barcelona na Hispania, Ansu Fati, yamekwama baada ya wakala wa kinda huyo mwenye umri wa miaka 18, Jorge Mendes, kutaka mkataba wa miaka miwili na kukataa kuwekwa kwa kipengele cha kuondoka kwa euro bilioni moja. **(El Nacional)**

### LIVER YATAKA NYOTA HISPANIA
MKURUGENZI wa Michezo wa Liverpool, Michael Edwards anawaniwa na Real Madrid ili kuisaidia klabu hiyo ya Hispania kwenye masuala ya uhamisho wa wachezaji. **(Sun)**

### VLAHOVIC LULU SPURS, NEWCASTLE
KLABU za Tottenham Hotspur na Newcastle United zinamwania mshambuliaji wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21. **(Sun)**

### HICKEY ATAKIWA VILLA
ASTON Villa imemweka katika orodha ya wachezaji inayowataka mlinzi wa kushoto wa Bologna, Aaron Hickey baada ya kuonyesha kiwango bora kwenye Serie A, lakini mlinzi huyo Mscotland mwenye umri wa 19 hana haraka ya kuondoka Italia. **(Sun)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA ANASTAHILI BALLON D'OR - ZIDANE

**Ni wakati sahihi kwa sababu yupo kwenye kiwango cha juu katika mchezo huu kwa sasa...**

**PARIS, Ufaransa**

KARIM Benzema anastahili kuwa Mfaransa wa kwanza kushinda Ballon d'Or tangu Zinedine Zidane - na maneno hayo yametoka kwa Zidane mwenyewe.

Straika huyo wa Real Madrid, Benzema, ambaye amechukua unahodha tangu kuondoka kwa Sergio Ramos aliyejiunga na Paris Saint-Germain, anacheza soka la kuvutia wakati akielekea kutimiza umri wa miaka 34, Desemba mwaka huu.

Zidane ameliona hilo kwa karibu, akiwa ametumia misimu miwili kama kocha wa Madrid akimshuhudia kwa uzuri zaidi Benzema.

Ingawa Zidane aliondoka hapo 'Los Blancos' mwishoni mwa msimu uliopita, anamwona Benzema kama anayestahili kubeba tuzo ya Ballon d'Or.

Akizungumza na TFI's Telefoot, Zidane alisema: "Tunazungumza kuhusu mchezaji ambaye anastahili kushinda Ballon d'Or.

"Ni mchezaji wa aina yake, nilikuwa na heshima kubwa sana kumnoa yeye. Anajua namna ya kufanya kila kitu dimbani.

"Natumaini anaweza kuthaminiwa kwa kipaji chake kwa kupewa Ballon d'Or. Ni wakati sahihi kwa sababu yupo kwenye kiwango cha juu katika mchezo huu kwa sasa."

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa amekuwa nguzo ya safu ya ushambuliaji ya Madrid tangu kuondoka kwa Cristiano Ronaldo aliyetua Juventus mwaka 2018 na kiwango chake kimekuwa cha kuvutia.

Mshindi wa Ballon d'Or atatangaza Novemba 29, mwaka huu katika sherehe zitakazofanyika jijini Paris.

MECHI KALI
HOME
PARIS ST GERMAIN
1.52 | 4.53 | 5.48
RB LEIPZIG
AWAY
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 595

# AGUERO ATOA NENO KUANZA KUKIPIGA BARCA



**BARCELONA, Hispania**

SERGIO Aguero amesema anafuraha kubwa kuanza kuichezea Barcelona wakati ikibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Valencia kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, pale Camp Nou, Jumapili.

Baada ya kukamilisha uhamisho wa bure kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City, Aguero alitumia zaidi ya miezi miwili akijiuguza kigimbi kabla ya kujumuishwa kwenye kikosi cha Ronald Koeman, Jumapili.

Aguero akiwa na jezi ya Barca kwa mara ya kwanza aliingia dimbani katika dakika ya 87 akichukua nafasi ya Sergino Dest muda mfupi baada ya Philippe Coutinho kufunga bao la tatu kwa miamba hao wa LaLiga.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina, Aguero alikuwa mchezaji wa tatu mwenye umri mkubwa zaidi kuanza kuichezea Barcelona kwenye LaLiga katika karne ya 21 (miaka 33 na siku 137), baada ya Lilian Thuram mwaka 2006 (miaka 34 na siku 251) na Demetrio Albertini mwaka 2005 (miaka 33 na siku 159).


Akiwa amerudi kwenye LaLiga kwa mara ya kwanza baada ya kuondoka Atletico Madrid kwenda Ligi Kuu England miaka 10 iliyopita, Aguero alipata mapokezi makubwa kwa kushangiliwa na mashabiki walioimba jina lake.

"Ndio, ulikuwa wakati wa kuvutia sana," alisema mfungaji huyo wa muda wote wa City akiiambia Barca TV.

"Watu wanaliita jina langu, wakiimba jina langu. Nilifurahi zaidi kuona hilo.

"Napenda kuwashukuru wote wakati nikiwa dimbani kwani walinipa hamasa kubwa. Siwezi kuwashukuru wao kwa mmoja mmoja, lakini nina matumaini walifurahia uwapo wangu uwanjani."

# Allegri asema sasa Juve ipo njia sahihi



**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri, amekubali alifanya baadhi ya "makosa" mwanzoni mwa msimu, lakini miamba hao wa Serie A wanaelekea kwenye njia sahihi baada ya kuifunga AS Roma.

Moise Kean alifunga bao pekee kwenye ushindi wa 1-0 wa Juve Jumapili nyumbani, huku Wojciech Szczesny akiokoa penalti ya Jordan Veretout.

Juve sasa imeshinda mechi nne mfululizo kwenye Serie A katika michezo sita ya mashindano yote, ingawa ilianza msimu wa 2021-22 bila ushindi kwenye mechi tatu - wakipoteza mbili mfululizo baada ya kutoka sare mchezo wa ufunguzi.

"Tuna wachezaji ambao wana uwezo wa kutengeneza mashambulizi ya kushtukiza," alisema Allegri - ambaye amerudi tena hapo Turin kwa mara ya pili akichukua nafasi ya Andrea Pirlo - akiiambia DAZN.

"Ni ushindi mzuri, ni hatua nyingine kwenye msimamo na maendelezo mazuri zaidi kwa msimu.

"Tunawakosa (Paulo) Dybala, (Matthijs) De Ligt, (Adrien) Rabiot, (Alvaro) Morata, lakini wakati kila mmoja anapocheza kwa molari kubwa hutakiwi kuruhusu mabao.

"Kwa sasa naona kwamba, tunakwenda kwenye njia sahihi kwa sababu tulianza vibaya na tulistahili ushindi kwenye mchezo huu."

HABARI MICHEZO

5,659,980

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/10/2021 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.33 | 3.41 | 3.01 |
| 02. 23/10/2021 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.37 | 3.16 | 2.97 |
| 03. 23/10/2021 | 17:00 | Peterborough vs QPR | 2.90 | 3.20 | 2.39 |
| 04. 23/10/2021 | 17:15 | Cadiz CF vs Alaves | 2.51 | 3.02 | 3.07 |
| 05. 23/10/2021 | 19:30 | Elche vs Espanyol | 2.71 | 3.02 | 2.82 |
| 06. 23/10/2021 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Villarreal | 2.53 | 3.14 | 2.93 |
| 07. 24/10/2021 | 14:00 | Nice vs Lyon | 2.63 | 3.47 | 2.53 |
| 08. 24/10/2021 | 16:00 | West Ham vs Tottenham | 2.38 | 3.36 | 2.96 |
| 09. 24/10/2021 | 16:00 | Brentford vs Leicester | 2.62 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 24/10/2021 | 17:15 | Barcelona vs Real Madrid | 2.65 | 3.54 | 2.53 |
| 11. 24/10/2021 | 18:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.36 | 3.44 | 2.84 |
| 12. 24/10/2021 | 18:30 | Manchester Utd vs Liverpool | 3.07 | 3.62 | 2.21 |
| 13. 24/10/2021 | 19:00 | Roma vs Napoli | 2.62 | 3.43 | 2.62 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 19 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3515 | Lokomotiv Plovdiv vs Pirin Blagoevgrad | 1.44 | 4.16 | 6.19 |
| 16:30 | 2942 | Tshakhuma vs Bloemfontein Celtic | 2.60 | 3.09 | 2.70 |
| 17:30 | 1014 | Celtic vs Ferencvaros TC | 1.62 | 4.10 | 5.01 |
| 18:30 | 5720 | TS Galaxy FC vs Amazulu | 2.85 | 2.85 | 2.65 |
| 19:45 | 2871 | Besiktas vs Sporting Lisbon | 3.11 | 3.31 | 2.29 |
| 19:45 | 3162 | Brugge vs Manchester City | 8.61 | 5.31 | 1.32 |
| 21:00 | 2087 | Al Nasr Riyadh vs Al Hilal Riyadh | 3.01 | 3.16 | 2.24 |
| 21:45 | 1210 | QPR vs Blackburn | 2.11 | 3.40 | 3.25 |
| 21:45 | 2010 | Stoke City vs Bournemouth | 2.83 | 3.07 | 2.53 |
| 21:45 | 2607 | Buxton FC vs Scarborough Athletic | 1.76 | 3.63 | 3.97 |
| 21:45 | 2612 | Mansfield vs Port Vale | 2.85 | 3.30 | 2.45 |
| 21:45 | 2685 | Kings Langley vs Harrow Borough | 3.11 | 3.59 | 2.02 |
| 21:45 | 2732 | Cheltenham vs Morecambe | 2.06 | 3.45 | 3.35 |
| 21:45 | 2772 | Salisbury City vs Chesham Utd | 1.80 | 3.63 | 3.78 |
| 21:45 | 2890 | Barrow vs Scunthorpe | 1.63 | 3.80 | 5.40 |
| 21:45 | 3059 | Merstham vs Bowers Pitsea | 2.13 | 3.80 | 3.05 |
| 21:45 | 3073 | Stratford Town vs Nuneaton | 1.97 | 3.65 | 3.60 |
| 21:45 | 3084 | Fleetwood Town vs Burton | 2.45 | 3.21 | 2.82 |
| 21:45 | 3246 | Leyton Orient vs Forest Green | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 21:45 | 3443 | Rushden and Diamonds vs Barwell | 2.12 | 3.53 | 2.95 |
| 21:45 | 3454 | Bristol City vs Nottingham | 2.71 | 3.10 | 2.61 |
| 21:45 | 3484 | Truro City vs Tiverton Town | 2.26 | 3.53 | 2.71 |
| 21:45 | 3500 | Harrogate vs Tranmere | 2.20 | 3.20 | 3.20 |
| 21:45 | 3941 | Needham Market vs Biggleswade Town | 2.27 | 3.52 | 2.70 |
| 21:45 | 4193 | Wigan vs MK Dons | 2.09 | 3.31 | 3.41 |
| 21:45 | 4306 | Derby vs Luton Town | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 21:45 | 4397 | Lincoln vs AFC Wimbledon | 2.20 | 3.25 | 3.20 |
| 21:45 | 4487 | Sheffield Utd vs Millwall | 1.80 | 3.40 | 4.43 |
| 21:45 | 4537 | Plymouth vs Bolton | 2.34 | 3.30 | 2.91 |
| 21:45 | 4613 | Colchester vs Bristol Rovers | 2.40 | 3.40 | 2.85 |
| 21:45 | 4670 | Northampton vs Stevenage | 2.10 | 3.20 | 3.44 |
| 21:45 | 4706 | Rotherham vs Wycombe | 1.81 | 3.55 | 4.14 |
| 21:45 | 4874 | Coalville Town vs Peterborough Sports | 2.38 | 3.62 | 2.51 |
| 21:45 | 4876 | Charlton vs Accrington | 2.05 | 3.31 | 3.50 |
| 21:45 | 5028 | Oxford Utd vs Shrewsbury | 1.73 | 3.49 | 4.72 |
| 21:45 | 5113 | Alvechurch vs Tamworth | 2.46 | 3.53 | 2.46 |
| 21:45 | 5147 | Sutton United vs Swindon Town | 2.22 | 3.30 | 3.25 |
| 21:45 | 5190 | Dorchester Town vs Hartley Wintney | 2.47 | 3.59 | 2.43 |
| 21:45 | 5807 | Portsmouth vs Ipswich | 2.18 | 3.20 | 3.30 |
| 21:45 | 5871 | Wimborne Town vs Weston Super Mare | 2.71 | 3.53 | 2.26 |
| 21:45 | 5965 | Merthyr Town vs Poole Town | 3.63 | 3.83 | 1.79 |
| 22:00 | 1672 | Porto vs AC Milan | 2.49 | 3.39 | 2.74 |
| 22:00 | 1768 | Inter vs Sheriff Tiraspol | 1.19 | 7.17 | 12.95 |
| 22:00 | 2721 | CD Santa Cruz vs Rangers | 2.09 | 3.19 | 3.29 |
| 22:00 | 3074 | Shakhtar Donetsk vs Real Madrid | 5.28 | 4.15 | 1.59 |
| 22:00 | 3566 | Paris St Germain vs RB Leipzig | 1.52 | 4.53 | 5.48 |
| 22:00 | 4635 | Atletico Madrid vs Liverpool | 3.15 | 3.30 | 2.27 |
| 22:00 | 5645 | Ajax vs Borussia Dortmund | 2.17 | 3.84 | 2.94 |
| 22:00 | 5963 | Tenerife vs Eibar | 2.44 | 2.91 | 3.11 |
| 22:45 | 1400 | Union Santa Fe vs Racing Club | 2.29 | 3.14 | 2.95 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MOURINHO AJITOA UKOCHA NEWCASTLE



**ROME, Italia**

JOSE Mourinho ameondoa uwezekano wa yeye kuwa kocha ajaye wa Newcastle United, lakini anatambua kwamba, "nina uhusiano wenye hisia" na jiji hilo.

Mourinho ambaye ni kocha wa zamani wa Chelsea, Manchester United, Tottenham Hotspur na sasa AS Roma, hafikirii kurudi tena kwenye Ligi Kuu England.

Baada ya Kampuni ya uwekezaji wa fedha za umma ya Saudi Arabian kuinunua timu hiyo ya St James' Park, mabadiliko mengi yanatarajiwa katika klabu hiyo.

Steve Bruce amebaki kuwa kocha mkuu kwa sasa, lakini uvumi umezagaa kuhusu hatima yake, huku wamiliki wapya wakiwa wanataka kocha mwenye rekodi kubwa.

Mourinho anaweza kufiti kwenye nafasi hiyo hasa kutokana na mafanikio aliyoyapata kwenye ligi za Ulaya pamoja na mashindano makubwa ya bara hilo.

Lakini alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kuhamia Newcastle, Mourinho amesema uwezekano huo kwa sasa haupo kwani ana mkataba na Roma, ambayo inamilikiwa na bilionea wa Marekani, Dan Friedkin.

Mourinho alihamia kwa klabu hiyo yenye maskani yake mji mkuu wa Italia, baada ya kutangazwa kuteuliwa Mei mwaka huu.

Amesema anahisia nzuri sana na jiji la Newcastle kwani ni sehemu anayoipenda, pia alikuwa na ushirikiano mzuri na Robby Robson wakati akiifundisha Barcelona ambayo baadaye alikwenda kuinoa timu hiyo ya Magpies.

"Kitu pekee ninachoweza kusema ni kwamba, kwa miaka mingi, mingi sana, nilifanya kazi na mtu ambaye ni muhimu zaidi katika historia ya Newcastle, Sir Bobby Robson," alisema Mourinho.

"Na kwa sababu ya hilo nimekuwa na uhusiano wenye hisia ya aina yake na jiji lile na mashabiki wake."

# Nagelsmann: Bayern ilistahili mabao zaidi



**MUNICH, Ujerumani**

JULIAN Nagelsmann aliridhishwa na kiwango cha Bayern Munich wakati wakiifumua Bayer Leverkusen mabao 5-1, lakini anahisi timu yake ilistahili mabao mengi zaidi.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, walijibu kipigo walichokipata kutoka kwa Eintracht Frankfurt wiki mbili zilizopita, kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia pale katika dimba la BayArena.

Robert Lewandowski na Serge Gnabry kila mmoja alifunga mabao mawili kipindi cha kwanza na Thomas Muller pia akafunga, mabao yote yakipatikana ndani ya dakika 37.

Hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Bayern kufunga mabao matano ugenini katika kipindi cha kwanza kwenye mchezo wa Bundesliga wakati wakirudi kileleni na kuitoa Borussia Dortmund.

Licha ya ushindi huo Nagelsmann anaona kwamba, timu yake ilistahili kushinda mabao mengi zaidi.

"Tulikuwa na nafasi ya kufunga mabao mengi zaidi kwani tulikuwa kwenye kiwango cha kuvutia sana," alisema Nagelsmann akiiambia DAZN.

# Michezo

Jumanne Oktoba 19, 2021
Nipashe



**Benzema anastahili Ballon d'Or - Zidane**

UKURASA 21

NIPO TAYARI...



Mshambuliaji hatari wa Yanga, Fiston Mayele, akiwa mazoezini Songea na timu yake wakijiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya KMC FC itakayopigwa Uwanja wa Majimaji leo. **PICHA: YANGA**

# NABI ATEMA CHECHE KIWANGO YANGA, KMC

●●●Wazitaka pointi tatu Majimaji leo, ajivunia kuimarika safu ya ulinzi, lakini Habib Kondo asema...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

YANGA itakwea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza kama ikishinda mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara leo kwenye Uwanja wa Majimaji Songea, mkoani Ruvuma dhidi ya KMC.

Timu hiyo inayoshika nafasi ya pili kwa pointi sita, inawania kuweka rekodi ya kushinda mechi ya tatu mfululizo, ambayo itawapeleka kuwa na pointi tisa, huku Polisi Tanzania inayoongoza hadi leo ikiwa haina mechi yoyote wiki hii.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wamejipanga vema kwenye mechi ya leo, na wana matarajio ya kupata ushindi, japo wanafahamu KMC ni timu ngumu.

"Tumejipanga vema, KMC siyo timu mbaya, natarajia utakuwa ni mchezo wenye ushindani," alisema Mtunisia huyo.

Furaha kwa wanachama na mashabiki wa Yanga ni urejeo wa wachezaji wawili, David Bryson na Yassin Mustapha ambao walikuwa majeruhi.

"Kwenye safu ya ulinzi hakuna matatizo kwa sababu Yassin na Bryson wamepona, hivyo watakuwa sehemu ya kikosi," alisema.

Alisema kazi kubwa aliyokuwa anaifanya ni kwenye eneo la ushambuliaji ambalo lilikuwa na tatizo.

"Nimekuwa mkali kidogo kwenye safu ya ushambuliaji na kuwataka wacheze kwa ushirikiano na siyo kila mtu acheze kwa ajili ya mafanikio yake binafsi," alisema kocha huyo baada ya kuona kuwa washambuliaji wake kila mmoja anataka kufunga yeye hata kama hayupo kwenye eneo zuri na linahitaji kutoa pasi.

Alisema wameona uwanja wanaocheza na wanatakiwa kuwa makini kuhakikisha wanaweza kupata matokeo mazuri katika mchezo huo ili kuendelea kujiimarisha katika nafasi za juu kwenye msimamo.

"Uwanja hautakuwa mzuri, tunatambua viwanja vingi si vizuri sana kama ilivyo ule wa Benjamini Mkapa, tunahitaji kupambana na hali hiyo, pamoja na aina ya timu tunakwenda kukutana nayo, timefanya maandalizi ya aina hii kuhakikisha tunapata matokeo chanya," alisema Nabi.

Naye Kocha Msaidizi wa KMC FC, Habib Kondo, alisema wamefanyia kazi mapungufu yao ikiwamo kuimarisha zaidi safu ya ulinzi kukabiliana na washambuliaji wa wapinzani wao hao.

"Hatutakuwa na mechi rahisi, kwa sababu kila mmoja anahitaji matokeo mazuri, tumeanza vibaya katika michezo miwili iliyopita kutoka sare moja na kufungwa mmoja, sasa hatuwezi kukubali kupoteza mechi hii ya nyumbani.

"Najivunia kikosi changu hakina mabadilko makubwa kwa sababu hatujafanya usajili mkubwa tofauti na Yanga, imefanya usajili mkubwa na wachezaji wengi wao ni wapya, itakuwa mechi ngumu na ushindani mkubwa," alisema kocha huyo.

Mechi nyingine zitakazopigwa leo ni Azam FC watakuwa nyumbani Uwanja wa Azam Complex, kuwakaribisha Namungo FC kutoka Ruangwa mkoani Lindi.

## Gomes aichambua mechi Simba, Galaxy

**Na Waandishi Wetu**

LICHA ya baadhi ya mashabiki na wadau wa soka kueleza kutovutiwa kwa soka liliiloonyeshwa na Simba wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 ugenini nchini Botswana dhidi ya Jwaneng Galaxy, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mfaransa Didier Gomes, amewapongeza wachezaji wake kwa kucheza kwa nidhamu kubwa kama alivyowaelekeza kufanya.

Katika mechi hiyo ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Taifa wa Botswana, mabao hayo ya Simba yalifungwa na Taddeo Lwanga na nahodha John Bocco.

Akizungumza na Nipashe jana, Gomes alisema hawakuwa na haja ya kucheza mpira wa kufurahisha mtu, badala yake walijua wanacheza ugenini na timu nzuri, hivyo lengo lao namba moja lilikuwa ni kupata ushindi.

"Hatukuwa na haja ya kucheza mpira wa kufurahisha watu, tulikuwa tunataka ushindi ambao ni muhimu kwenye michuano hii, tulicheza kwa nidhamu. Tuliifunga mechi kwa kucheza kwa nidhamu kubwa.

"Hatukutaka kuruhusu bao ili kupunguza matumaini yao kwenye mechi ya marudiano na tuliwaheshimu kwa sababu wanacheza kwenye ardhi yao ya nyumbani. Tuliona itakuwa ni faraja kubwa kwa wanachama na mashabiki wa Simba kwanza kuingia angalau kwenye makundi ya Ligi ya Mabingwa," alisema kocha huyo.

Kuhusu mabao mawili ya mapema, yote yakiwa ya kona, kocha huyo alisema kuwa jambo hilo halikuja kwa bahati mbaya, bali walifanyia kazi mazoezi.

Simba ambayo ilirejea jijini Dar es Salaam jana saa 10:00 alfajiri ikitokea moja kwa moja Botswana, sasa inahitaji ushindi au sare yoyote ama kutokubali kufungwa zaidi ya bao moja kwenye mechi ya marudiano Jumapili wiki hii ili kutinga hatua ya makundi.

**Habari hii imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Shufaa Lyimo**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042